# Nipashe

Ijumaa Desemba 25, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580440

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710


**JPM** asisitiza viongozi wa umma fomu za maadili

UKURASA 2



**MAWE** ya dhahabu yanaswa yakitoroshwa kwa kutumia trekta

UKURASA 3



BOSI TALGWU MWANZA:
Waajiriwa Serikali Mtaa wote mkoani tunao, walitimuliwa 300 tukawarejesha

BUFE

IJUMAA DESEMBA 25, 2020 Nipashe BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Ukurasa 12

Walimu wawili wanafundisha shule nzima

PROF: OLE GABRIEL

Katibu Mkuu Mifugo na darasa la ng'ombe wa 'Uchumi wa Kati'

•DC Musoma adaka na kunadi kwake

Na Sabato Kasika

KUFIKA uchumi wa kati, maana yake Tanzania imeingia uchumi wa viwanda. Wafugaji wanakumbushwa kuacha kufuga kienyeji, sasa wahamie stadi za kisasa kupata mazao yenye ubora kwa matumizi ya viwandani.

Ni ufugaji upi? Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Elisante Ole Gabriel, anautaja ni kuhimilisha mifugo kupata maziwa mengi, nyama nyingi na ngozi bora kwa ajili ya viwandani.

"Wafugaji wanatakiwa kufuga kisasa, kwa ajili ya kuwaongezea kipato, kwa kutumia teknolojia ya uhimilishaji, ambayo inayomwezesha mfugaji kuchagua mbegu bora ya ng'ombe mwenye uwezo wa kutoa maziwa mengi," anaeleza.

Profesa Ole Gabriel, anasema teknolojia ya uhimilishaji, inaruhusu ng'ombe kupandikizwa bila dume na kupata mbegu bora ya ng'ombe ...

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Elisante Ole Gabriel. PICHA: MTANDAO

... mgeni kwa wafugaji wengi, hivyo ni muhimu kuwapa elimu waelewe, ili iwe rahisi kukubali teknolojia hiyo yenye manufaa makubwa kwao," anasema mkuu wa wilaya.

Anaendelea kwamba, kuna wafugaji wanaofurahi milki ya makundi makubwa ya ng'ombe, hivyo ni muhimu kuelimishwa wabadilike, akitoa mfano wanalazimika kuhama kila msimu kutafuta maji na malisho na hata wanaangukia migogoro kati yao na wakulima.

"Ninaamini kwamba, wafugaji wote wakizingatia maelekezo ya wizara na kutumia teknolojia ya uhimilishaji, watapata faida kubwa kuliko kuendelea kuzunguka na ng'ombe wengi wenye faida ndogo," anasema.

Inaelezwa Tanzania ilipopata uhuru mwaka 1961, ilikuwa na ng'ombe milioni tisa, lakini sasa wameongezeka hadi milioni 30.5, huku idadi ya watu nayo ikiongezeka kutoka milioni 10 ya wakati huo hadi milioni 55 wa sasa.

Kwa mujibu wa Rais Dk. John Magufuli, katika moja ya mikutano yake ya hadhara, alitamka: ""Mifugo inaongezeka, watu wanaongezeka, shughuli zikiwamo za kilimo nazo zinaongezeka.

UKURASA 11

## RIPOTI MAALUM

# Shule yakumbwa ufuska wa kutisha

UKURASA 4



Mpambaji akipamba kibanda mfano wa alipozaliwa Yesu ndani ya Kanisa la Mtakatifu Alban, jijini Dar es Salaam, jana, ikiwa ni maandalizi ya Sikukuu ya Krismasi inayosherehekewa leo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wahukumiwa kunyongwa hadi kufa mauaji Mawazo CHADEMA

UKURASA 2

## YALIYOMO


**UKURASA WA 3**

### LATRA YATOA VIBALI MAGARI 80 VYA USAFIRISHAJI ABIRIA SIKUKUU

KATIKA kukabiliana na ongezeko la abiria wanaosafiri kwenda mikoa ya Kaskazini, Mamlaka ya...

**UKURASA WA 5**

### RC ATANGAZA KUKAMATWA MRAMBA KISA KODI ARDHI

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ametangaza...

**UKURASA WA 17**

### MWINYI ASIMAMISHA KAZI VIGOGO ZSSF

MKURUGENZI Mwendeshaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Sabra Issa Machano, na watendaji wengine...


## TCRA yaonya wanaopoteza laini za simu bila kuripoti

UKURASA 2


MICHEZO **YANGA: TUNA JAMBO LETU** UK. 24

**MAONI, KATUNI UK. 6**

# JPM asisitiza fomu maadili

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amewasisitiza viongozi wote wa umma takribani 15,000 wanaotakiwa kujaza fomu za maadili, kufanya hivyo kabla ya Desemba 30, 2020.

Rais Magufuli alisema hayo jana wakati akimwapisha Sivangilwa Mwangesi (Jaji wa Mahakama ya Rufani) kuwa Kamishna wa Maadili.

Alisema ndio maana amemteua Kamishna wa Maadili, Mwangesi kujaza nafasi iliyoachwa na Marehemu Nsekela ili kusiwe na visingizio.

Taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Gerson Msigwa, ilisema hafla ya kuapishwa kwa Mwangesi ilifanyika Ikulu, Chamwino, mkoani Dodoma na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali.

Akisisitiza kuhusu kujaza fomu hizo za maadili, Rais Magufuli ameitaka Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi kuchagana na ujazaji na uwasilishaji wa fomu za maadili ya uongozi kwa njia ya mtandao, ili kuepusha uvujaji wa siri na ubadilishaji wa maudhui ya fomu hizo, na badala yake zichukuliwe mtandaoni na kisha kujazwa na kuwasilishwa nakala halisi katika ofisi husika.

Akizungumza baada ya kumwapisha na kushuhudia Mwangesi akila kiapo cha uadilifu kwa viongozi wa umma, Rais Magufuli amemtaka kwenda kuendeleza kazi nzuri iliyofanywa na mtangulizi wake marehemu Jaji mstaafu wa Mahakama ya Rufani, Harold Nsekela.

Viongozi wengine waliohudhuria sherehe hiyo ni Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deo Ndejembi, Makatibu Wakuu na Naibu Katibu Mkuu, viongozi wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama na Kaimu Jaji Mfawidhi wa Mahakama ya Rufani Kanda ya Dodoma, Latifa Mansour.

Pia, Rais Magufuli amewatakia Watanzania wote heri ya Krismasi na Mwaka Mpya na ametaka viongozi na watumishi ambao hawana zuio la Waziri Mkuu kuruhusiwa kwenda makwao kusalimu ndugu na jamaa wakati huu wa sikukuu.



Rais Dk. John Magufuli akimkabidhi nyenzo za kazi Jaji Sivangilwa Mwangesi, baada ya kumwapisha kuwa Kamishna wa Maadili katika hafla iliyofanyika Ikulu Chamwino jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Waliomuua Mawazo wahukumiwa kunyongwa hadi kufa

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita imewahukumu watu wanne kunyongwa hadi kufa kwa kupatikana na hatia ya mauaji ya kukusudia ya aliyekuwa Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Mkoa wa Geita, Alphonce Mawazo, ambaye alikuwa mgombea wa ubunge Jimbo la Busanda, mwaka 2015.

Hukumu hiyo ilitolewa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Geita yenye mamlaka ya nyongeza kutoka Mahakama Kuu Kanda ya Mwanza, shauri la mauaji namba 9/2019.

Waliohukumiwa kunyongwa hadi kufa ni Alfan Apolinari (41), Epafula Zacharia (39), Hashimu Sharifu (45) na Kululinda Bwire (31), wote wakazi wa Katoro, mkoani Geita.

Washtakiwa wote kwa pamoja walifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita, majira ya saa 8.00 mchana na kupandishwa kizimbani saa 9:15 alasiri, mbele ya Naibu Msajili Mahakama Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza ambaye ni Hakimu Mkazi Mwandamizi Mwenye Mamlaka ya ziada, Frank Mahimbali.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na mawakili watatu, Javelin Rugaihuruza, ambaye ni Wakili wa Serikali Mkuu, Hezron Mwasimba, Wakili wa Serikali Mwandamizi na James Pallangyo, Wakili wa Serikali.

Upande wa washtakiwa uliongozwa na mawakili wa kujitegemea watano ambao ni Yisambi Siwale, Flora Enosy, Laurent Bugoti, Abel Sizya na Paul Hombo.

Hukumu hiyo ilitolewa baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo la mauaji ya kukusudia pasipokuacha shaka yoyote.

Hakimu Mahimbali alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya washtakiwa hao ili iwe fundisho kwao na kwa watu wengine wenye tabia za kikatili kama yao.

Alisema upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Rugaihuruza, ulipeleka mahakamani mashahidi 13 na vielezo vinane ambavyo vilithibitisha kuwa washtakiwa wote kwa pamoja walimuua Alphonce Mawazo kwa kukusudia.

Hakimu Mahimbali alisema upande wa utetezi ulipeleka mahakamani mashahidi watatu na vielelezo vitatu pamoja na utetezi wa washtakiwa wanne.

Alisema ushahidi uliotolewa na upande wa Jamhuri kwa shahidi namba nne na shahidi namba tisa, ulisema waliona tukio hilo majira ya mchana washtakiwa wakiwa na marungu, mapanga, fimbo na moko wakimshambulia Alphonce Mawazo.

Alisema ushahidi huo unawatia hatiani washtakiwa wote kwa pamoja na watanyongwa mpaka kufa.

Umati wa watu ulifurika mahakamani hapo huku askari polisi wakiwa na mabomu pamoja na silaha za moto kuhakikisha usalama unaimarika.

Baada ya hukumu hiyo washtakiwa wote waliangua vilio pamoja na ndugu zao waliofika kusikiliza, huku askari polisi wakiwatawanya ndugu hao eneo la mahakama.

Katika kesi hiyo, mshtakiwa Habibu Feruzi, aliachiwa huru baada ya ushahidi uliotolewa dhidi yake kuwa dhaifu na upande wa Jamhuri kufunga ushahidi wake.

Akisoma hati ya mashtaka, Msaidizi wa Kumbukumbu Mahakama Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza, Martina Nelei, alidai kuwa Novemba 14, 2015 katika Kijiji cha Rudete, Mkoa wa Geita, washtakiwa wote kwa pamoja walimuua mtu mmoja aliyefahamika kwa jina la Alphonce Mawazo.

# TCRA yaonya wanaopoteza simu

**Na Ndalike Sonda,** BARIADI

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Kanda ya Ziwa, imewataka wananchi kutoa taarifa wanapopoteza simu au laini zao, ili kuepukana na masuala ya uhalifu ikiwa mtu ataitumia vibaya.

Tahadhari hiyo ilitolewa jana mjini hapa na Ofisa wa Fedha wa TCRA Kanda ya Ziwa, Abdul Hussen, alipozungumza na Nipashe na kuongeza kwamba taarifa za kupotelewa simu ni muhimu kutolewa polisi.

Alisema sheria inamtambua mmiliki wa simu kuwa ndiye mwenye matumizi ya simu hiyo, hivyo anapopoteza au kuibiwa ni vyema kutoa taarifa polisi ili kujiweka salama.

"Ni kosa kisheria kupoteza laini ya simu halafu usitoe taarifa ya kupotelewa, maana simu yako ikitumiwa katika masuala ya uhalifu au makosa ya kimtandao, wewe utawajibika. Lakini kama umetoa taarifa itasaidia kukulinda. Nawashauri kutekeleza wale wanaopotelewa," alisema Hussen.

Naye Mhandisi Kulwa Masolwa kutoka TCRA Kanda ya Ziwa, aliwakumbusha wananchi kutotumia simu au laini ya mtu bila idhini yake kwa kuwa inaweza kusababisha kutiwa hatiani na kusababisha kufungwa.

Aidha, alisema TCRA imeweka utaratibu wa mafundi simu kuanzisha umoja wao kila wilaya na mkoa ili kuwapatia vyeti vya kuwatambua.

HABARI KITAIFA

# Mawe ya dhahabu yanaswa yakitoroshwa kwa trekta

**Na Happy Severine,**
BARIADI

JESHI la Polisi mkoani Simiyu kwa kushirikiana na Idara ya Madini mkoani hapo, limekamata mifuko 70 ya mawe ya dhahabu iliyokuwa ikisafirishwa kwa kutumia trekta bila kibali kutoka mgodi wa Dutwa kwenda Bariadi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Simiyu, Richard Abwao, alisema walikamata trekta hilo aina ya Swaraj lenye namba za usajili T 125 AZK likisafirisha mawe ya dhahabu bila kuwa na kibali.

Alisema walimkamata dereva wa trekta hilo, Elisha Maduhu (28) na meneja wake, Hussein Makoye (35) wote wakazi wa Bariadi na kwamba wanashikiliwa katika kituo kikuu cha Polisi Bariadi pamoja na vielelezo vyao likiwamo trekta na mawe hayo.

"Taratibu za kisheria zinaendelea juu ya watu hawa. Zikikamilika watafikishwa mahakamani kwa mujibu wa sheria. Pia vielelezo vyote tunavishikilia likiwamo trekta na mawe yanayodhaniwa kuwa ni ya dhahabu," alisema.

Kamanda Abwao aliongeza kuwa katika uchunguzi walibaini trekta hilo lilikuwa na kibali cha mifuko minne kutoka kampuni ya EMJ iliyoko mgodi wa Dutwa, huku mifuko mingine ikiwa haina kibali.

Ofisa Madini Mkoa wa Simiyu, Oscar Kalowa, alisema trekta hilo lilikamatwa Jumatatu iliyopita usiku likisafirisha mawe ya dhahabu kutoka mgodi wa Dutwa kwenda Bariadi.

"Baada ya kuwakamata walituonyesha kibali cha mifuko minne toka kampuni ya EMJ, lakini mfuko mingine 70 haina kibali wala nyaraka zozote. Dereva na meneja walisema si wahusika wa mzigo huo," alisema Kalowa.

Alisema watuhumiwa hao watafunguliwa jalada la utoroshaji wa mawe na kwamba sheria ya madini iko wazi kuwa mzigo utataifishwa sambamba na faini au kifungo nje ya faini.

Kalowa aliongeza kuwa watuhumiwa watafikishwa mahakamani ambapo sheria ya madini inakaziwa na mahakama kulipa faini au kifungo au vyote kwa pamoja.

Aliwataka wananchi kuacha mara moja kufanya biashara haramu ya kutorosha mawe na kwamba wachimbe kwa kufuata taratibu za madini ili mapato ya serikali yapatikane.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimkabidhi ripoti ya Mradi wa ZUSP Mkurugenzi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA), Mussa Haji Alikwa, kwa ajili ya kuifanyia kazi wakati wa mkutano wake na wafanyakazi wa mamlaka hiyo, uliofanyika Ofisi za Idara Victoria Garden Zanzibar. **PICHA: IKULU**

# LATRA yatoa vibali magari 80 vya usafirishaji abiria sikukuu

**Na Christina Mwakangale**

KATIKA kukabiliana na ongezeko la abiria wanaosafiri kuelekea mikoa ya Kaskazini, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA), imetoa vibali kwa magari 80 kusafirisha abiria kutoka Dar es Salaam kwenda mikoa ya Kaskazini, ikiwamo Kilimanjaro, Tanga na Arusha.

Meneja Leseni kutoka LATRA, Leo Ngowi, aliimbia Nipashe jana kuwa kati ya mabasi hayo, 42 yanakwenda Kilimanjaro, Arusha (15), Tanga (9), Rombo (5), Same (3), Malinyi (2), Bumbuli (2), Handeni (6).

Alisema mikoa ya Morogoro na Dodoma kuna ongezeko la wasafiri na kwamba yaliyopo yanakidhi mahitaji, huku Mkoa wa Lindi ukiongezewa mabasi mawili.

"Kuna ongezeko la abiria husussan mikoa ya Kaskazini, mbali na vibali kutolewa tumeongea na wenzetu wa Shirika la Reli (TRC) mchana (jana) huu kuna treni itakayobeba abiria zaidi ya 500 kwa safari ya Kilimanjaro," alisema Ngowi.

Aidha, mwanzoni mwa wiki hii, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Gilliard Ngewe, akizungumza na moja ya redio, alisema kutokana na ongezeko la mahitaji ya usafiri Kanda ya Kaskazini, wametoa vibali maalumu kwa kampuni binafsi za usafirishaji ili kutoa huduma hiyo.

"Kama kuna walio na mabasi ya kuweza kusafiri Arusha, Kilimanjaro tunatoa vibali vya muda kwa muda wa siku saba, hili ndio suluhisho kwa sasa," alisema Ngewe.

Kikubwa mabasi au Coaster zikaguliwe kama yanaweza kufika safari za huko, wakaguzi wayakague kabla ya kuanza safari, dereva pia athibitishwe anaweza kufika safari za mbali sio ambaye amezoea udereva wa safari za Dar es Salaam tu," alisema Ngewe.

# Polisi adaiwa kujeruhi kisa wivu wa mapenzi

**Na Amon Mtega,** SONGEA

JESHI la Polisi mkoani Ruvuma linamshikilia askari wake, Konstebo Keneth Mkwela, kwa tuhuma za kumjeruhi Andrew Milanzi (33) kwa kutumia kitu chenye ncha kali kwa kile kilichodaiwa kuwa wivu wa kimapenzi.

Kaimu Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Kamishna Msaidizi (ACP) Pili Mande, alisema tukio hilo lilitokea wiki iliyopita majira ya saa 6:00 usiku katika Kijiji cha Magagula Wilaya ya Songea kwenye nyumba ya wageni baada ya kubaini kuwa Milanzi alikuwa akifanya mawasiliano na mwenza wake.

Mande alisema askari huyo anadaiwa kumchoma raia huyo na kitu chenye ncha kali katika eneo la chini ya ubavu wa kushoto na kumsababishia maumivu makali ambayo yamesababisha kulazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Ruvuma mjini hapa.

Alisema kutokana na madai ya kutenda kitendo hicho, askari huyo ataendelea kushikiliwa na

Jeshi la Polisi wakati akisubiri taratibu za kisheria pamoja na taratibu za kiaskari katika kipengele cha nidhamu kwa askari.

Kamanda huyo pia alielezea mafanikio yaliyofanywa na jeshi hilo katika msimu wa mwaka 2020 ikiwamo kuteketeza ekari 49.5 za bangi, miche 13,053 ya bangi na kilo 280.3, huku watuhumiwa 124 wakichukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Pia alisema lita 359,125 za pombe haramu ya gongo zilikamatwa, mitambo miwili ya kutengenezea pombe hiyo pamoja na watuhumiwa 33 walikamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Kuhusu nyara za serikali, alisema watuhumiwa 21 walikamatwa wakiwa na miguu miwili, utumbo wa nyati na vipande 30 vya nyama ya kuro, vipande 26 vya nyama ya ngorombwe, vipande 21 vya meno ya tembo na vipande 25 vya nyama ya nguruwe pori.

Kamanda pia alisema jeshi lilikamata bunduki mbili aina ya Shotgun na gobole na watuhumiwa wawili huku watuhumiwa watatu walikamatwa na mali idhaniwayo kuwa ya wizi yakiwamo mafuta ya dizeli lita 120 na mafuta ya kula aina ya Oleo Miaia ndoo 178 zenye ujazo wa lita 10 kila moja.

Kwa upande wa usalama barabarani, alisema kumekuwa na ajali 39 na ajali zilizosababisha vifo 27 watu 42 walifariki kati yao wanaume sita na wanawake 36 na ajali zilizosababisha majeruhi ni 12 na kusababisha majeraha kwa watu 57 kati yao wanaume 44 na wanawake 13.

RIPOTI MAALUM

# Shule yakumbwa ufuska wa kutisha

## ■Mabinti ndugu vinara wa kambi
## ■Wavulana nao na uchafu wao

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

UNAPOZUNGUMZIA nidhamu ya mwanafunzi, moja kwa moja unamgusa mwanafunzi katika weledi wa utii wa sheria, maelekezo na miongozo shuleni na jamii kwa ujumla.

Lakini mtu anapofuatilia hilo kwa wanafunzi wa shule moja iliyoko wilayani Siha mkoani Kilimanjaro, yanayojiri toka kwa vijana hao yanapishana kwa asilimia zote na tafsiri iliyotangulia.

Je, mtu anaweza kuamini mustakabari wa shule kugeuka uwanja uliotukuka wa ngono, tena ukibeba uchafu ambao hata ni mgumu kupata nafasi ya kutamkwa mdomoni?

Fuatilia simulizi; Ofisi ya Ustawi wa Jamii, ambayo hasa ndiyo mwenyeji mfuatiliaji, inaanza na dokezo la kuwapo mabinti wa shule ya msingi ambao usiku kwao haupiti pasipo kulala na mwanamume.

Pia, kaka zao wa kiume shuleni nao wamehalalisha ya kwao, matendo machafu ya aina hiyo katika mfumo kinyume cha maumbile.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya hiyo, Peter Msaka, anadokeza aliyonayo mkononi kupitia uchunguzi wa awali kwamba wasichana wawili ndugu, kati ya wanafunzi 17 ndiyo manahodha wa madhila hayo, tena akisisitiza wenza wao ni watu wazima.

Ni mkasa unaokuja katika hitimisho la mwaka, huku Nipashe mwanzoni mwa mwaka huu ilifahamishwa na Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Watoto katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mwajuma Magwiza, namna hali hiyo inavyoshika kasi kitaifa.

Katika kikao walichoandaa na walimu wa Siha kujadili kasoro za kijamii zinazojitokeza miongoni mwa vijana wao, Msaka anasema bado wako kwenye hatua za kuwahoji ingawa tayari wameshaibua mengi.

"Tulipokea taarifa ya shule moja ya msingi ambayo sitaitaja jina kwa sababu bado tunaendelea kufanyia kazi taarifa ambazo tumezipata.

"Pale kuna wanafunzi 17. Kati yao, tumekuta taarifa za kujihusisha na mapenzi kati ya wanafunzi kwa wanafunzi, ambao sasa imefika wakati pia hao wanafunzi wanalawitiana.

"Yaani, kuna mapenzi ya jinsia moja kwa watoto wa kiume, lakini pia kuna wa kiume na wa kike.

"Tumekwenda pale na tumekaa nao katika hali ya urafiki, tumezungumza kwa kina, lakini ukiangalia katika wale wanafunzi 17, ni wanafunzi wawili tu wanaishi na wazazi.

"Hawa wanafunzi 15 wanaishi na ndugu kama babu, bibi na dada," ofisa huyo anasimulia, katika staili




Wanaharakati wa kutetea ulinzi na usalama wa watoto dhidi ya vitendo vya kihalifu, kama vinavyotokea kwa wanafunzi wa wilayani Siha. **PICHA: MTANDAO**



Ofisa Ustawi wa Jamii Wilaya ya Siha, Peter Msaka. **PICHA: GODFREY MUSHI**

ya kuanika mashila ya aina yake yanayojiri mahali hapo.

**NINI KIFANYIKE?**

Mwanasaikolojia na mtaalamu wa magonjwa ya akili, Johari Hassan, anataja hatua stahiki ya kuanzia ni kufanyika anachokitamka kitaalamu kwamba ni 'assessment' au tathmini.

Johari anasema ni jambo linalofungua msingi wa tatizo kwa kuzingatia kitaalamu, maumbile ya kila mtu ana yana upekee wake.

Anaendelea: "Kwa hiyo tiba yake inategemea na mtu binafsi. Sasa hao wanafunzi hawawezi kufanana watoto wote 17.

"Kuna wengine watafika mbali mpaka watahitaji tiba ya dawa na siyo saikoloji tu.

"Labda anajihusisha na kitendo hicho kwa sababu ana maradhi fulani ya magonjwa ya akili, ambayo yanachochea na kumfanya anakuwa na msukumo wa kujihusisha na tendo la ngono.

"Mwingine ni mazingira, ni suala la saikolojia, ni mazingira aliyopo ndiyo yamemkuta na kumsukuma kufanya ngono katika umri mdogo."

Johari ambaye ni Mratibu wa Afya ya Akili wa Wilaya ya Siha, anaweka angalizo la hisia ya kitaalamu kwamba, huenda wanafunzi hao wanajiingiza katika ngono kutokana na masuala ya kifamilia.

Mtaalamu huyo anaenda mbali katika sura ya pili kwamba pia huenda wakawapo wanaoshawishiwa na mazingira ya makazi.

Ili kuwasaidia, Johari anasema kunahitajika huduma ya kisaikolojia itakayosaidia kukabili mtazamo walionao kiakili, kwa kuwa hadi sasa wanaamini wanachokitenda ni haki yao na kuwaingilia ni kuwafanyia hujuma.

**POLISI JE?**

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Ronald Makona, alipotafutwa na Nipashe kutolea ufafanuzi wa kisheria suala hilo alitamka:

"Hata mimi nimelisikia hilo tukio, lakini halijaripotiwa kwetu. Kinachotakiwa hapo ni waliripoti tupate taarifa ya msingi ili tuwe na sehemu ya kuanzia, ingawa watu wa Ustawi wa Jamii wanaweza kuendelea kulichunguza, kwa sababu wanaruhusiwa kisheria kupata undani wa tukio lenyewe linalohusiana na ukatili."

Mratibu wa Mradi wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Watoto na Wanawake (MTAKUWWA) wilayani Siha, Peter Mashingia, ana ufafanuzi kuhusu namna wanavyokabiliana na matukio ya namna hiyo.

Anataja eneo mojawapo ni kujenga uwezo kwa walimu, akitaja kwa sasa kuna shule 12 zinazosimamia klabu za watoto kupinga unyanyasaji wa kingono.

**HALI ILIVYO KITAIFA**

Mwanzoni mwa mwaka huu, Nipashe ilizungumza na Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Watoto katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mwajuma Magwiza, aliyekiri kukithiri kwa matukio hayo.

Mwajuma alifafanua kwamba tatizo la ulawiti dhidi ya watoto nchini ni kubwa na lipo katika maeneo mengi.

"Zamani vitendo kama hivi vilikuwa ni siri, watu walikuwa wanaogopa kutoa taarifa, lakini huenda tunaona kwamba vimeongezeka kwa sababu watu wanatoa taarifa kwa wingi sasa hivi," alisema.

Alibainisha kwamba kwa takwimu zilizoishia Desemba mwaka jana, Mkoa wa Tanga ulikuwa unaongoza kwa vitendo hivyo wakati Mkoa wa Dar es Salaam uliongoza kwa madhila hayo mwaka 2018.

Katika kukabiliana na tatizo hilo, mkurugenzi huyo alisema tayari wameanzisha kampeni 'Twende Pamoja', inayoendeshwa nchi nzima, ikilenga kutoa elimu ya kukomesha vitendo hivyo.

"Tunashirikiana na halmashauri zote na madawati ya jinsia, tunatoa elimu ya kupambana na kuvikomesha," alisema.

Wakili wa Sheria, Leonard Manyama, huku akirejea vifungu kadhaa vya sheria, anaeleza sheria za nchi zinavyoelekeza adhabu kali mpaka kifungo cha maisha kwa wanaothibitika kuhusika na ubakaji pia ulawiti dhidi ya watoto.

## HABARI KITAIFA

# Wasichana 300 kupatiwa elimu Ukimwi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

HALMASHAURI ya Mji wa Makambako mkoani Njombe kwa kushirikiana na Shirika lisilo la kiserikali la Umbrela of Woman and Disabled Organization (UWODO), wanatarajia kuwafikia wasichana zaidi ya 300 wenye umri kati ya miaka 14 hadi 25, mwakani kwa ajili ya kuwapa elimu ya virusi vya Ukimwi (VVU).

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo mratibu wa Ukimwi Halmashauri ya Mji wa Makambako, Vaileth Ngesi, alisema kwa kuwa hali ya maambukizi bado inaendelea kupanda, kwa kushirikiana na wadau katika kutoa elimu itasaidia kupunguza kasi ya maambukizi.

"Hali ya maambukizi bado inaendelea kupanda hivyo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kama wenzetu wa UWODO tunaamini kabisa maambukizi yataendelea kupungua, tunawashukuru sana wenzetu kwa kutufikia kwa sababu pia watatoa elimu lishe kwa wasichana," alisema Ngesi.

Mmoja wa vijana mkazi wa mjini Mkambako, Vashti Kifuso, alisema vipo vishawishi vingi vinavyosababisha vijana kuingia kwenye ngono katika maeneo yao ikiwamo mwingiliano wa wafanyabiashara pamoja na wasafirishaji wa mizigo, huku wakiomba elimu iendelee kutolewa dhidi ya maambukizi ya virusi vya Ukimwi.

"Upo umuhimu wa kuendelea kutuelimisha watoto wa kike kujikinga na ugonjwa hatari la Ukimwi kwa sababu hapa Makambko kuna vishawishi vingi sana na hii itatuepushia na maambukizi na hata wazazi wetu wamekuwa wakiendelea kutupatia elimu hata tunapokuwa tunaenda hospitali," alisema Kifuso.

Naye Zaeli Ngigwa alisema; "Kuna umuhimu kutoa elimu na wazazi ifike mahala waelimishe watoto bila woga juu ya janga la Ukimwi na ninashauri tuendelee kujihadhari na mabinti nao wajitahidi kubadilika hata kwenye mavazi," alisema Ngigwa.

Mkurugenzi wa Shirika la UWODO, Hamis Kassapa, alisema mradi huo unatarajia kutekelezwa katika kata tatu za mji wa Makambako kwa muda wa mwaka mmoja mpaka Desemba 2021, ukiwa umefadhiliwa na ubalozi wa Marekani kupitia Mfuko wa Rais PEPFA.

"Tuko hapa kwa ajili ya uzinduzi wa mradi wetu wa uhamasishaji kwa wasichana kushiriki katika upimaji wa virusi vya Ukimwi mradi utatekelezwa kwa muda wa mwaka mmoja kwenye kata za Mjimwema, Mwembetogwa pamoja na Ubena," alisema Kasapa.

"Tutafanya kazi na wasichana kwasababu hapa Makambako kuna makutano ya magari yanayokwenda nchi za jirani na kuna wakati madereva wanapumzika hapa huku wengine wakiwatumia wasichana na tumeona wasichana wako kwenye hatari kubwa sana ya kushawishiwa na hatimaye kuingia kwenye ngono, huku wengine wakiambukizwa na VVU," alisema Kasapa.



Wavuvi wa Bwawa la Nyumba ya Mungu wakimwonyesha Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul (kulia), samaki aina ya perege waliovuliwa katika bwawa hilo, baada ya kumaliza kuongea na wavuvi hao, wilayani Mwanga, mkoani Kilimanjaro juzi. **PICHA: MBARAKA KAMBONA**

# RC atangaza kuwakamata Mramba, wenzake

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ametangaza kuwakamata na kuwaweka ndani baadhi ya vigogo akiwamo waziri wa zamani katika serikali za awamu ya kwanza hadi ya nne, Basil Mramba, kutokana na kugoma kulipa kodi ya ardhi.

Chalamila aliyasema jana jijini hapa mbele ya waandishi wa habari kuwa Mramba na wenzake wameshindwa kulipa kodi kwenye vitalu vya ranchi ya Usangu wilayani Mbarali kwa miaka 17.

Mbali na Mramba, aliwataja vigogo wengine kuwa ni Mbunge wa zamani wa Mbarali, Estelina Kilasi, na aliyewahi kuwa Mwenyekiti wa Shirika la Ndege la Precision Air, Michael Shirima.

Wengine ni Dk. Emmanuel Swain na Charles Kaaya ambao wanatoka kwenye kampuni ya ALL and Sea Company Ltd, Henry Bwire na Fred George ambao wanatoka kwenye kampuni ya SLIGHT Tanzania Ltd.

Pia wamo Jaji Antony Mrema, Jorobi Shein, Malembo Bundala, Saida Bundala, Mahembo Bundala na Njingo Bundala, Ng'wandu Mahola na Konde Mahona ambao wanatoka Kampuni ya Mahola Ranch Company Ltd.

Alisema viongozi hao pamoja na kampuni zilizomilikishwa vitalu kwenye ranchi hiyo, wanadaiwa zaidi ya Sh. bilioni 1.7 ambazo walitakiwa kuilipa serikali kama kodi ya pango la ardhi tangu mwaka 2007.

"Tumeamua kuwasaka popote walipo watu hawa ambao tunawadai fedha hizi, majina yao tunayo na ni wengi lakini vinara hasa ambao tutaanza nao ni pamoja na Mramba, Shirima na Kilasi," alisema Chalamila.

"Nawahakikishieni kuwa tutawakamata bila kujali vyeo vyao na watachukuliwa hatua kali za kisheria," alisisitiza.

Katika kutekeleza hilo, alisema kuanzia leo vyombo vya dola vitaizingira ranchi ya Taifa ya Mifugo ya Usangu kuzuia ng'ombe wote waliomo wasitoke na kusema wahusika hawatalipa fedha hizo mpaka leo saa 3:00 asubuhi, mifugo hiyo itataifishwa na serikali. Alisema ranchi hiyo ina vitalu 16 ambavyo wadaiwa hao walimilikishwa kihalali mwaka 2007 na kupatiwa hati ya umiliki ya miaka 33, lakini tangu wakati huo hawajawahi kulipa kodi ya pango la ardhi kwa mujibu wa sheria.

Alisisitiza kuwa yeye ndiye waziri wa wizara zote ndani ya mkoa, hivyo lazima ahakikishe kila sekta inaendeshwa kwa kufuata sheria, huku akidai kuwa wakuu wa mikoa kazi yao ni kumsaidia rais kuwahudumia wananchi.

Chalamila alisema baada ya uchunguzi kwenye kampuni zinazodaiwa fedha hizo imebainika kuwa wako pia baadhi ya viongozi ambao bado wamo kwenye utumishi wa umma na wengine wamo ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Alisema taarifa hizo pia atazifikisha kwa Katibu Mkuu wa CCM, ili ikiwezekana baadhi ya wahusika wachukuliwe hatua za kinidhamu kwa mujibu wa kanuni za chama.

# NHIF yaonya udanganyifu

**Na Rose Jacob,** MWANZA

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), umeshtukia watoa huduma za afya wanaozidisha bili kwa lengo la kufanya udanganyifu ili walipwe fedha nyingi tofauti na huduma wanazotoa kwa mgonjwa. Kutokana na hali hiyo, mfuko huo umetangaza kuwachukulia hatua za kisheria watoa huduma watakaofanya hivyo ili kukomesha vitendo hivyo.

Akizungumza katika kikao cha wadau wa mfuko huo uliowashirikisha watoa huduma wa sekta binafsi na serikali chenye lengo la kujadili changamoto mbalimbali, Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernad Konga, alisema tatizo hilo linasababisha ucheleweshwaji wa malipo kwa watoa huduma waaminifu.

Konga alikiri kwamba siku za nyuma kulikuwa na malalamiko kuhusu ucheleweshaji wa malipo kwa watoa huduma mbalimbali nchini, lakini kwa sasa mfuko umefanya maboresho na sasa malipo yanatoka kwa wakati.

Alisema watoa huduma katika mfuko huo, wanaopaswa kuacha tabia ya kuongeza bili ili walipwe fedha nyingi na kwamba atakayebainika serikali itamchukulia hatua za kisheria. Meneja wa NHIF, Mkoa wa Mwanza, Jarlath Mshashu, alisema watoa huduma wanatamani kuona uongozi wa mfuko huo unawatembelea. Aliongeza kuwa mfuko huo umeendelea kufanya kazi mbalimbali ikiwamo kusajili wanachama, vituo vya kutolea huduma, kukusanya michango, kulipa madai ya watoa huduma, kutoa elimu kwa wadau wa mfuko na kutengeneza kadi za wanachama.


## NOTISI / TANGAZO

NUTMEG AUCTIONEERS AND PROPERTY MANAGERS CO.LTD, CHAMPION AUCTION MART LTD, SUNDI AUCTION MART LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, MASETO AUCTIONEERS AND DEBT COLLECTORS LTD, BESTGROUP LTD SALEI AUCTION MART LTD, kwa Mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC**, tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili,Vinginevyo, tutafanya minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| S/No | JINA LA MTEJA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | FLUGENCE GERVAS KIMARIO | FLUGENCE GERVAS KIMARIO | NYUMBA YENYE HATI MILIKI NO.40675, KIWANJA NO.542, BLOCK "E" | SOKONI ONE-ARUSHA | 11/01/2021. NAKUENDELEA |
| 2. | GREEN USANGU GENERAL ENTERPRICES | FRANCIS MASUMBUKO MBILINYI | NYUMBA, KWENYE KIWANJA NA.1114 KITALU 'Z' | ISYESYE - MBEYA | 11/01/2021. NAKUENDELEA |
| 3 | MARRY BURTON KIMANGA | FRANK ZUBERI MWASIKILI | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | KIJIJI CHA MPANDA KIWIRA –MBEYA | 16/01/2021 NAKUENDELEA |
| 4 | KIBA AMON MANIAMBA | KIBA AMON MANIAMBA | PLOT NO.2482, "BLOCK Y" | MWAKITEBE AREA - MBEYA | 11/01/2021. NAKUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika,Na 75% itakayo baki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwamnunuziatashindwakutimizashartilolotelamnadakuhusiananamalipoyaawali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. 0754497396 /0719922700.
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Noeli njema, tusherehekee tukijiepusha na bala

**KESHO** ni sikukuu ya Noeli, tunawatakia wasomaji wetu na Watanzania wote, sikukuu njema na ya heri, tukiwasihi wazazi na walezi wasisahau kuwalinda watoto wao, nao wajilinde ili kuwaepusha na majanga yanayoweza kusababishwa na kujisahau.

Pamoja na kuwakumbusha kujilinda tunawahimiza kujiepusha na ajali zinazoweza kusababishwa na kutumia usafiri wenye mashaka kama bodaboda, bajaji, Noah na bajaza tukiwarundika watoto wetu na wanafamilia wengi ndani ya chombo au vyombo hivyo.

Tunawashauri kama ikiwezekana tushiriki ibada na tutulie nyumbani ili iwe siku ya familia kwa kuwa hizo ndizo nyakati za kukaa pamoja na familia zetu.

Ni vyema kuchukua tahadhari kwa kuwa usafiri usio rasmi wa kubeba watu wengi kwa wakati mmoja unaweza kuhatarisha maisha ya watoto hasa wakati wa sikukuu kama Noeli na Mwaka Mpya, hivyo tujihadhari.

Taarifa ya Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), iliyochapishwa kwenye gazeti letu la jana, inaonyesha kuwa ajali za pikipiki zilizoripotiwa hospitalini hapo kwa miaka 10 iliyopita kuanzia 2010 hadi 2020 ni takribani 60,000 kwa hiyo si usafiri salama sana hasa wakati huu ambao madereva wanaendesha wakiwa na fikra za kusaka pesa zinazotokana na wengi kuhitaji huduma yao wakati huu wa sikukuu.

Mwaka 2018, MOI, ilieleza kuwa inapokea majeruhi wa ajali za bodaboda takribani 20 kila siku na kuufanya uwezekano wa watu 600 kujeruhiwa au kufa kila mwezi na piki piki hivyo tahadhari ni muhimu.

Ukweli ni kwamba kuruhusu bodaboda kuwasafirisha watoto wakati kama huo wa sikukuu unaweza kufananishwa na kuwatumbukiza kwenye midomo ya mamba.

Pamoja na kwamba wakati huu wa sikukuu ni muda wa kupata fursa, za kuhudumia wateja wengi, lakini ni vyema kuwalinda watoto na wanafamilia wote ili fursa hiyo isiwe na athari kwao.

Hii ni kwa sababu wapo madereva wanaojilipua kwa kunywa pombe nyingi, baadhi wanachanganya vileo vya aina mbalimbali wapo pia ambao huvuta bangi na mihadarati mingi, tena baadhi wanatamba kuwa wamejilipua, kwa hiyo wazazi na walezi na wana familia chungeni watoto wenu na jamaa yote.

Mwaka 2018, MOI, ilieleza kuwa inapokea majeruhi wa ajali za bodaboda takribani 20 kila siku na kuufanya uwezekano wa watu 600 kujeruhiwa kila siku na pikipiki.

Ukweli ni kwamba ni lazima kuwa makini tunapotumia bodaboda kuwasafirisha watoto wakati kama huo wa sikukuu kunaweza kufananishwa na kuwatumbukiza kwenye midomo ya mamba.

Pamoja na kwamba wakati huu wa sikukuu ni muda wa kupata fursa, za kuhudumia wateja wengi, lakini ni vyema madereva wakawa makini lakini kila upande kuwalinda watoto na wanafamilia wote ili fursa hiyo isiwe na athari kwao.

Ni vyema tunapokwenda kwenye ibada za usiku tukaweka makazi yetu kwenye hali ya usalama kwa kufunga na kuwa na uangalizi wa wanyama wetu.

Tukiwa kwenye maeneo ya ibada na sehemu za starehe tukumbuke kulinda mali zetu hasa vyombo vya usafiri kama magari, pikipiki na bajaji kwa vile kuna wahalifu wanaotumia nyakati hizo kuiba.

Kila la kheri, tusisahau kuwa na tahadhari na kulinda maisha na kuwajali wengine.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge

# Umakini unahitajika kwa watoto leo sikukuu na mwaka mpya ujao

Na Maulid Mbaga

**NCHINI** Tanzania na sehemu nyinginezo duniani, leo imetimu sikukuu kama ilivyo ada ya kila ifikapo mwishoni mwa mwaka watu kusherehekea Krismasi na Mwaka Mpya.

Kama inavyofahamika watu wanasheherekea kwa namna mbalimbali, kulingana na mahali walipo, ikiwamo kutembelea sehemu za vivutio na wengine kwenda katika majumba ya starehe na kadhalika. Watoto nao si haba, wanatembea huku na kule kutimiza azma ya furaha zao.

Miaka iliyopita zilipofika nyakati kama hizi za sikukuu ina kawaida kuripotiwa matukio mbalimbali yanayoripotiwa kuhusu upotevu wa watoto kutokana na uzembe wa kuachwa wakatembea wenyewe mitaani, bila ya uangalizi maalumu.

Watanzania wanapaswa kujifunza kutokana na matukio yaliyokwishatokea kuwa makini na watoto hususani pale wanapoamua kuwaruhusu watembee, waweke uangalizi maalumu kwa ajili ya usalama wao.

Kadhalika, Watanzania wanashauriwa kuzitumia siku hizo kusherehekea kwa kufanya mambo yanayowaletea faida katika siku zijazo na kujiepusha na yote yanayoashiria uvunjaji wa sheria.

Kwa wakazi wa mijini, ndio wapo katika maeneo yanayohitaji uangalizi mkubwa kwa watoto kwani wanakuwa na utaratibua wa kwenda sehemu nzenye mikusanyiko ya watu wengi, jambo ambalo pasipokuwa na mtu makini wa kuwasimamia ni rahisi kupotea na kusababisha usumbufu.

**Kwa wakazi wa mijini, ndio wapo katika maeneo yanayohitaji uangalizi mkubwa kwa watoto kwani wanakuwa na utaratibua wa kwenda sehemu nzenye mikusanyiko ya watu wengi, jambo ambalo pasipokuwa na mtu makini wa kuwasimamia ni rahisi kupotea na kusababisha usumbufu.**

Hivyo, wazazi wote wanapaswa kuelewa umuhimu wa huzingatia usalama wa watoto wao hususani nyakati ambazo watoto wanatoka nje ya mazingira ya nyumbani.

Aidha, kwa upande wa wanaoandaa sehemu za kuchezea watoto ikiwa ni moja ya kukamilisha furaha ya watoto katika kusherehekea sikukuu, wanapaswa kuweka utaratibu maalumu wa kuwazuia watoto wasidhurure, bila ya utaratibu au mwongozo.

Kama ilivyo ada kwa upande wa maofisa wa Polisi, kuwahusia wazazi mara kwa mara kuhakikisha, usalama wa watoto wao wanapotoka majumbani hasa kwa kipindi kama hicho cha sikukuu.

Maofisa wa Polisi wamekuwa wakifanya kazi kubwa ya kuwakumbusha wazazi, sambamba na wao wenyewe kuhakikisha kuna usalama wa raia na mali zao.

Pia, litakuwa jambo zuri endapo Jeshi la Polisi litaelekeza nguvu zaidi katika maeneo yanayotazamiwa kuwa na msongamano mkubwa wa watu katika kipindi hiki cha sikukuu, ili kuwahakikishia usalama wao.

Vilevile Watanzania wanakumbushwa kuwa makini na mali zao kwani nyakati kama hizi ndipo vitendo vya wizi hushamiri, ikiwamo kuvunjiwa majumbani, pia na kuporwa mikoba na vibaka barabarani.

Katika kipindi cha sikukuu kumekuwapo matukio ya uporaji, hususani katika maeneo mbalimbali ndani ya Jiji la Dar es Salaam, hivyo wakazi wa jiji hilo na mingine kwa ujumla inayoripotiwa kuwa na vitendo vya namna hiyo, wanakumbushwa kuwa makini hasa nyakati hizi za mwisho wa mwaka.

Kadhalika ni jukumu la kila Mtanzania kuhakikisha anakuwa makini na mienendo yake na kujiepusha na vitendo vya uvunjaji wa sheria vinavyoweza kumsababishia matatizo yasiyokuwa na ulazima.

HABARI KITAIFA

# Wakurugenzi waagizwa kutenga fedha za mifugo

**Na Mbaraka Kambona,** KILIMANJARO

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul, amewataka wakurugenzi wa halmashauri zote nchini kutekeleza waraka wa mwaka 2002 unaowataka kutenga asilimia 15 ya mapato yanayotokana na shughuli za Sekta ya Mifugo na Uvuvi na kuzirejesha kwenye sekta hizo, ili kuboresha shughuli zake.

Alitoa agizo hilo alipokuwa akiongea na viongozi wa Wilaya ya Mwanga, mkoani Kilimanjaro alipotembelea kukagua shughuli za sekta hiyo zinazotekelezwa wilayani humo, Desemba 23, 2020.

Kwa mujibu wa Gekul, mwaka 2002 serikali ilitoa waraka ambao unaelekeza kuwa halmashauri zote nchini zihakikishe kuwa mapato yanayopatikana kutokana na shughuli za sekta ya mifugo na uvuvi itengwe asilimia 15 na zirudishwe kwa sekta hizo, ili kuboresha huduma kwa mifugo ikiwamo ukarabati wa majosho, minada na kununua chanjo za mifugo. "Wakurugenzi rejeeni huo waraka ambao unadumu mpaka mwaka 2025, ili mtekeleze kama ulivyoagiza na tukifanya hivyo itasaidia kuboresha huduma za mifugo yetu na tupate mazao bora yanayotokana na mifugo hiyo," alisema Gekul.

Vilevile, alisema miundombinu mingi ya kuhudumia mifugo imechoka akitoa mfano wa minada ya kuuzia ng'ombe kuwa mingi haina uzio, mifugo inauzwa katika maeneo ya wazi, jambo ambalo linachangia upotevu wa mapato ya halmashauri.

"Najua katika halmashauri zetu mara nyingi fedha huwa hazitoshi, lakini ni muhimu kujenga nidhamu ya matumizi ya fedha na tukifanya hivyo itakuwa rahisi kutenga hizo pesa ili kuboresha sekta za mifugo na uvuvi, hivyo naagiza baada ya kutoka hapa tukatekeleze hilo," alisisitiza Gekul.

Waziri Gekul alisema, mwelekeo wa serikali kwa sasa ni kuhakikisha majosho yanaboreshwa, minada inakarabatiwa na chanjo zinapatikana kwa urahisi, ili wananchi wasihangaike kupata huduma kwa ajili ya mifugo yao.

Pia, aliwataka maofisa mifugo kuhakikisha wanasimamia vyema ukusanyaji wa maduhuli ya serikali ili kuzuia upotevu wa mapato kwa kuwa makusanyo yakiwa mazuri na huduma za mifugo zitaboreshwa.



Kamanda wa Polisi mkoani Arusha, ACP Salum Hamduni, akionyesha silaha aina ya pistol browning zilizokamatwa na jeshi hilo, baada ya kufanikiwa kuwaua watuhumiwa wawili wa ujambazi. **PICHA: TUMAINI MAFIE**

# Waziri aonya wanaochochea migogoro wakulima, wafugaji

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amewaonya baadhi ya viongozi wa vijiji na kata wanaoshirikiana na wafugaji kuvunja sheria kwa kuwanyanyasa wakulima katika maeneo yao.

Ndaki alisema baadhi ya viongozi wa vijiji badala ya kuwa watatuzi wa migogoro wamegeuka kuwa wachochezi na kusababisha iendelee wakitafuta maslahi yao binafsi kutoka kwa makundi hayo.

Alisema viongozi wa vijiji watakaobainika kushiriki katika kuchochea migogoro hiyo, watachukuliwa hatua.

Alisema serikali haiko tayari kuvumilia viongozi wanaotengeneza migogoro katikati ya jamii, ili wao wanufaike na kuwaacha wananchi wakiumia.

"Siku zote wakulima na wafugaji wamekuwa ni jamii zinazoelewana kwa sababu kila mmoja amekuwa akihitaji huduma kutoka kwa mwenzake, kwa maana ya mazao ya kilimo na mifugo, lakini inapotokea tena eti baadhi ya viongozi wa vijiji wanaingiza chuki kati yao na kuwachonganisha kwa maslahi binafsi, hili ni tatizo na ni hatari na sisi hatuwezi kuvumilia haya," alisema Ndaki.

"Serikali haitaangalia nani ni mpole na nani mkali, kundi lolote ambalo tutalibaini kwamba ndilo chanzo cha migogoro tutaliadhibu, tunataka kila mtu afuate au kuendesha shughuli zake kwa kufuata sheria za nchi na si vinginevyo na tukifanya hivyo itatusaidia kuishi pamoja kwa upendo."

Aliwataka wafugaji kushirikiana na serikali kujenga miundombinu ya ufugaji yakiwamo malambo ya maji ya kunyweshea mifugo yao husussani katika maeneo ambayo wamekabidhiwa na serikali kufuga.

"Mahitaji ya wafugaji ni mengi, wanahitaji malambo, malisho, majosho na minada katika maeneo yao wanayofugia, kwa hiyo ni vyema tukishirikiana," alisema Ndaki.

Alisema katika bajeti ijayo, wizara hiyo ina mpango wa kutenga kiasi cha fedha kwa ajili ya kujenga malambo katika maeneo mbalimbali nchini kuanzia katika baadhi ya vijiji kwa kushirikiana na halmashauri.

"Tunataka kuhakikisha sekta hii inakuwa chachu ya maendeleo katika nchi yetu, tutahakikisha kwamba tunaweka miundombinu mizuri ambayo itasaidia kufikia katika malengo makubwa ya uzalishaji tunayoyataka katika nchi yetu," alisema Ndaki.

Mwisho

# Mbunge aliyechomewa nyumba, atoa ya moyoni

**Na Mwandishi Wetu,** LIWALE

MBUNGE wa Liwale, Zubeir Kuchauka, amekutana na wananchi wa jimbo lake na kueleza jinsi tukio la kuchomewa nyumba na magari lilivyomwathiri katika kipindi cha uchaguzi mkuu, Oktoba 28.

Kachauka ambaye alikutana na wananchi hao, kuwashukuru kwa kumchagua na kusikiliza kero zao, aliwataka kuacha makundi na kujenga Liwale kwa umoja wao kwa kuwa siasa za makundi na visasi hazijengi bali zinasababisha uhasama na utengano. Akizungumza Liwale katika viwanja vya Nanjinji, Kuchauka alisema yeye alikuwa mwathirika wa kuchomewa nyumba, magari matatu kipindi cha uchaguzi na kueleza kuwa tukio hilo lilimsikitisha na kuwataka sasa wananchi kusahau yaliyopita na kuchapa kazi.

Katika tukio hilo baadhi ya watuhumiwa wanashikiliwa na Jeshi la Polisi.

Kachauka alisema Wanaliwale ni wamoja na wanatakiwa kuwaza na kufanya mambo ya msingi kwa mustakabali wao, badala ya kuwaza mambo ya vurugu na uvunjifu wa amani.

"Si mmeona nguvu hizo ambazo wananchi wanazozifanya kuchoma nyumba na gari la serikali ni kwa sababu hakuna nguvu zao walizowekeza na kusema tu mali ya serikali, lakini kama wangechangia au wangechangia nguvu ya kujenga shule au hospitali hakuna mtu angefanya uovu huo kwa kuhofia nguvu zake kupotea," alisema.

"Basi tushirikiane kuanza sisi ujenzi wa shule hospitali ya wilaya halafu serikali inawekeza nayo nguvu zake humo tunasaidiana kujenga na sio kubomoa," alisema.

Awali, alitoa nafasi kwa wananchi kuuliza maswali na kuelezea changamoto zao ambazo zingine zilipatiwa majibu papo hapo na viongozi waliokuwapo na kuhusika na mengine kuahidi kushughulikia.

Baadhi ya kero ni pamoja na huduma za afya kwa upande wa kinamama eneo la upasuaji kuwa na upungufu wa vyumba wakati idadi ya wazazi ikiwa kubwa kutokana na mji huo kukua kwa kasi. Sharifa Mwenyeji, alimweleza mbunge huyo kuwa kero kubwa ni ya ununuaji vifaa vya upasuaji kwa ajili ya kujifungua.

"Kwanza tuna kero ya kulala wawili wawili kitandani wakati wa kujifungua, pia kutakiwa kufika na vifaa kufanyiwa operesheni hata kama hufanyiwi na ukijifungua bila operesheni vifaa vyote unaviacha hapo," alisema Sharifa.

Wananchi pia walilalamikia ukosefu wa umeme wa REA katika vijiji 37.

Isaya Kitoweli, alimuomba mbunge kufikisha kero zao hasa ya kujengewa kituo kidogo cha polisi kwa ajili ya kudhibiti kwa haraka matukio ya uhalifu.

Baadhi ya wananchi walililamikia kukosa maeneo ya ujenzi wa nyumba za kuishi na wamehakikishiwa na Mwenyekiti wa Halmashauri, Mohamed Mtesa, kuwa tatizo hilo limekwisha kwa kuwa linaendelea kutatuliwa.

Kero zingine ni pamoja barabara kutoka Nangurukuru mpaka Liwale, ambalo alisema ndio kipaumbele kwa sasa.

## Wanafunzi kushiriki kambi sayansi Tanga

**Na Christina Mwakangale**

WANAFUNZI 70 kutoka shule za umma na binafsi nchini, wanatarajia kushiriki kambi ya siku tano yenye lengo la kukuza uhamasishaji wa masomo ya sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati (STEM).

Kambi hiyo iliyoandaliwa na Projekt Inspire, Shirika la Ufadhili la Botnar na Halmashauri ya Jiji la Tanga, inatarajia kufanyika jijini Tanga kuanzia Desemba 28 hadi Januari Mosi, mwakani.

Ofisa Programu Msaidizi wa kampuni hiyo, Kelvin Joseph, alisema malengo yao ni kumwamsha kijana kiakili ili kufanya uamuzi sahihi wa taaluma utakaomfaa baada ya kuhitimu masomo.

"Kambi hii itazingatia uwakilishi wa jinsia, kutokana na tatizo lililopo kwa wasichana, tangu shuleni ni wachache wanaosoma masomo haya ndiyo maana wahandisi wanawake ni wachache," alisema Joseph.

Alisema wakati wa kambi hiyo, wanafunzi watapata fursa ya kujifunza kuhusu taaluma mbalimbali na kuwahamasisha kuwa na matamanio na ndoto zao.

"Hatua hii inawawezesha wanafunzi kubuni na kupewa ujuzi wa utafiti muhimu katika maendeleo ya nchi, hasa katika wakati huu wa mapinduzi ya sayansi na teknolojia kwa Tanzania iliyojikita katika uchumi wa viwanda," alisema Joseph.

Alisema miaka minne iliyopita, Projekt Inspire imeandaa kambi nne ambazo zimewanufaisha zaidi ya vijana 500 nchini kupitia ushiriki wa kambi hizo na klabu zilizoko shuleni. Joseph alisema ujumbe wa mwaka huu ni 'Wasichana na Wavulana katika STEM kwa Maendeleo Endelevu, Kukahikisha Mafunzo ya Sayansi Teknolojia, Uhandisi na Hisabati Jumuishi na yenye Usawa kwa Mafunzo Endelevu'.

"Leo katika zama mpya ya teknolojia, dunia iko katika njia panda. Kuna mabadiliko makubwa kwa namna tunavyoishi, namna tunavyofanya kazi, jinsi uchumi na biashara zinavyotengenezea sura mpya ya uchumi na jamii katika miaka ijayo.

Mapinduzi ya kiteknolojia yanatoa fursa kubwa kwa nchi ambazo zina uwezo wa kuzitumia," alisema Joseph. Meneja Masoko wa kampuni hiyo, Ronnue Godfrey, alisema mafunzo hayo kwa awamu ya tano sasa yametoa mwamko kwa wasichana kushiriki kambi hiyo.

"Dhana iliyopo kwenye jamii hata wanawake kuwa masomo ya sayansi, hisabati hatuyawezi tuiondoe, msichana tangu ukiwa shuleni unatakiwa kuweka nia ya dhati kwamba ninaweza masomo yote," alisema Ronnie.

# Gwajima ataka vipaumbele tiba maeneo yasiyofikika

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, amewaagiza waganga wakuu wote wa mikoa kuweka vipaumbele kuboresha huduma za afya katika maeneo yote ambayo hayafikiki kwa urahisi ikiwamo visiwani.

Dk. Gwajima alitoa agizo hilo jana mjini hapa alipokuwa katika ziara ya siku moja mkoani Pwani na kuzungumza na Mkuu wa Mkoa wa Pwani na kutembelea Hospitali ya Rufani ya Tumbi.

Alitoa agizo hilo baada ya kupokea maombi kutoka kwa Mhandisi Ndikilo ya kuboresha huduma za afya ikiwamo dawa na madaktari kwa wilaya ya Mafia ambako wanakumbana na tatizo la usafiri kwa kufuata huduma za afya jijini Dar es Salam.

Gwajima alisema waganga wakuu hao wanatakiwa kuainisha maeneo hayo ambayo jiografia yake ni kikwazo kwa wananchi kusafiri kutafuta huduma za afya ili yatafutiwe ufumbuzi wa haraka.

Pia alisema atatembelea katika kisiwa cha Mafia na kukagua huduma za afya, kuongea na wataalamu, ili afahamu vikwazo vinavyowakabili katika utoaji wa huduma na kutafutiwa ufumbuzi.

Kuhusu mrundikano wa wagonjwa katika Hospitali ya Mkuranga, Gwajima aliahidi kushughulikia tatizo hilo kwa kufika hospitalini hapo sambamba na kutatua tatizo la dawa kwenye vituo vya afya ambavyo vimekuwa vikilalamikia kukosa dawa.

Awali, Ndikilo alimweleza Waziri huyo kuwa Wilaya ya Mafia inakabiliwa na uhaba wa madaktari na kumwomba kusaidia upatikanaji wa wataalamu wa mionzi hasa katika Hospitali ya Ikwiriri ambayo tayari ina vifaa vya mionzi.



Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Mwigulu Nchemba, akipokea vitabu vya miongozo kwa Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Jaji Dk. Eliezer Mbuki Feleshi, baada ya kufanya mazungumzo na Menejimenti ya Mahakama, ikiwa ni siku tatu ya ziara ya kikazi jijini Dar es Salaam juzi. PICHA: **MPIGAPICHA WETU**

# Wawili wauawa tuhuma ujambazi

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

JESHI la Polisi mkoani Arusha limewaua watu wawili waliokuwa wanatuhumiwa kwa ujambazi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Salum Hamduni, alisema jana kuwa tukio la kuuawa kwa watu hao lilitokea Desemba 24 mwaka huu majira ya saa 7:10 usiku baada ya washukiwa hao kudaiwa kujaribu kurushiana risasi na askari polisi.

Kamanda Hamduni alisema: "Tukio lilitokea baada ya mtuhumiwa mmoja aitwaye Joseph Bernard kukamatwa na baada ya mahojiano, alikiri kuhusika katika matukio mbalimbali ya unyang'anyi na uvunjaji, alikubali kuonyesha watuhumiwa wenzake wanaoshirikiana nao ambao walikuwa wamepanga kuvamia duka la miamala ya pesa maeneo ya Sakina kwa Idd."

Aliongeza kuwa Jeshi la Polisi liliweka mtego na kutumia mbinu ya kumwachia mtuhumiwa huyo kwa lengo la kufanikisha ukamataji wa wenzake, jambo ambalo mtuhumiwa alitumia fursa hiyo kuanza kukimbia na kutoa ishara kwa wenzake kuwa kuna askari eneo hilo.

"Watuhumiwa hawa walianza kurushiana risasi na askari wetu lakini walijibiwa mapigo na kufanikiwa kuwajeruhi wawili na wengine walikimbia, lakini hawa majeruhi walifariki dunia wakiwa wanapelekwa hospitalini," Kamanda Hamduni alidai.

Aliwataja waliofariki dunia kuwa ni Joseph Bernard (24) na mwingine ambaye bado hajafahamika jina, akikadiriwa kuwa na umri wa kati ya miaka 30-34.

Alisema miili yao imehifadhiwa Hospitali ya Rufani ya Mt. Meru huku akibainisha kwamba jitihada za kuwatafuta watuhumiwa wengine zinaendelea.

Alisema jeshi hilo pia lilifanikiwa kukamata silaha aina ya Pistol Browning namba A080455-07 ikiwa na risasi nne, nyingine ni namba CZ75P-07 yenye risasi tano, maganda matatu ya silaha aina ya Shotgun pamoja na maganda sita ya silaha aina ya Pistol.

## Polisi yaonya wananchi vitendo vya ushirikina

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

JESHI la Polisi mkoani Rukwa limewataka wananchi kuwa makini na baadhi ya watu ambao wamekuwa wakipita katika nyumba zao na kufukia mapembe ya ng'ombe na vitu vingine.

Watu hao wamedaiwa kufanya hivyo ili kipindi cha kiangazi waanze kufukua wakidai kuwa ni vitu vya kishirikina waliwekewa na majirani zao ambao si wazuri.

Onyo hilo lilitolewa juzi na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rukwa, Justine Masejo, alipokuwa akizungumza na wakazi wa Bonde la Ziwa Rukwa wakati Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa ilipofika katika vijiji vya bonde hilo kuwatembelea watu ambao nyumba zao zilibomoka kutokana na mvua kubwa zinazonyesha mkoani hapa.

Alisema kuwa katika kipindi hiki cha mvua, kuna kundi la watu ambao wamekuwa wakipita katika nyumba za wananchi na kufukua ardhi kisha kufukia mapembe ya ng'ombe na vitu vingine vinavyoonekana kama vya kishirikina.

Kamanda Masejo alisema baada ya kufukia vitu hivyo kwa siri wanaondoka halafu watarudi kipindi cha kiangazi na kujifanya wao ni waganga wa jadi maarufu kwa jina la 'lambalamba' kisha kuanza kufukua vitu hivyo kwa madai ya kulipwa fedha, ili wasafishe nyumba kwa kuwa kuna vitu vya kichawi vimewekwa na majirani wasiowatakia mema.

Sambamba na hilo, Kamanda Masejo aliwakumbusha wakazi wa mkoa wa Rukwa kuwa waangalifu katika kipindi hiki cha sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya kwa kuwa baadhi ya watu wamekuwa wakitumia kipindi hiki kufanya uhalifu.

Pia aliwaonya wamiliki wa vyombo vya moto kuwa makini wanapokuwa barabarani na kuepuka kuendesha vyombo hivyo wakiwa wametumia vilevi kwa kuwa imekuwa sababu kubwa ya ajali zinazotokea mara kwa mara.

# Matukio ya ujambazi yamchefua RC

**Na Thobias Mwanakatwe**

MKUU wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali Nicodemus Mwangela, amelitaka Jeshi la Polisi mkoani humo kudhibiti mtandao wa majambazi ulioibuka hivi karibuni na kufanya matukio ya uporaji kwa kuvamia vituo vya mafuta na maduka.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi Brigedia Mwangela alisema licha ya hali ya usalama kuwa nzuri na kutokuwapo kwa kitisho chochote hasa kuelekea sherehe za Krismasi na Mwaka Mpya, amelitaka Jeshi la Polisi kujipanga na kukabiliana na matukio ya ujambazi wa kuvamia vituo vya mafuta na maduka ya wafanyabiashara.

"Kumekuwapo na matukio ya uvamizi na uporaji katika vituo vya mafuta na maduka makubwa ya wafanyabiashara katika miji ya Tunduma, Mlowo na maeneo mengine mkoani hapa, hivyo nimeagiza Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine kuhakikisha wanayakomesha mara moja," alisema.

Brigedia Mwangela aliyataja baadhi ya matukio hayo kuwa ni lile lililotokea katika kituo cha kuuza mafuta katika mji wa Tunduma ambalo majambazi haoo walipora kupora kiasi kikubwa cha fedha huku akisita kutaja kwa kuwa uchunguzi wa tukio hilo unaendelea.

Ingawa hakuwa tayari kutaja kiwango cha fedha na mali zilizoporwa, taarifa kutoka katika baadhi ya vyanzo vya zilidai mbali ya fedha, majambazi hao walipora silaha iliyokuwa ikitumiwa na walinzi wa kituo hicho.

Mbali na tukio hilo, Mkuu wa Mkoa aliyataja matukio mengine ya uvamizi kuwa ni yale yaliyotokea katika miji ya Mlowo na kambi ya Wachina.

Mwengela alitumia nafasi hiyo kuwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa vyombo vya dola kuwafichua wale wote wanaojihusisha na matukio ya kihalifu hasa wakati huu wa kuelekea mwisho wa mwaka.



Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, akifunga mita ya maji kuashiria kuanza kwa huduma ya maji kwa wananchi wa Tabata Kifuru kupitia mradi wa maji Pugu -Gongo la Mboto uliokamilika hivi karibuni. Kwenye ziara hiyo aliongozana na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abubakar Kunenge, Mbunge wa Segerea Bonna Kamoli na viongozi wengine wa DAWASA. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAKUKURU yaonya matumizi mabaya fedha

**Steven William,** MUHEZA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) wilayani Muheza, imewatahadharisha watumishi wa serikali na madiwani kuhusu ubadhirifu wa fedha za umma.

Imesema mtumishi au kiongozi atakayebainika kutumia fedha za serikali bila utaratibu atachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwamo kuburuzwa mahakamani.

Onyo hilo lilitolewa juzi na Kamanda wa TAKUKURU Wilaya ya Muheza, Christine Mkango, wakati akitoa elimu kwa madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza na watumishi wa halmashauri hiyo katika ukumbi wa Tate Plus, mjini hapa.

Alisema kumekuwa na tabia ya baadhi ya madiwani na watumishi kupokea fedha za serikali kwa wanachodai kwenda kufanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo vijijini, lakini hawafiki katika miradi husika, hivyo kutumia fedha za serikali bila kuzifanyia kazi kitendo ambacho ni kosa kwa mujibu wa sheria.

Mkango alisema: "Utakuta madiwani wengine hawajakaa katika kikao cha kamati au baraza la madiwani halafu baadaye wanapewa posho wanasaini (wanatia saini).

Hilo ni kosa kubwa kabisa, ikibainika umefanya hivyo diwani basi utachukuliwa hatua kali za kuiibia serikali."

Kamanda huyo wa TAKUKURU alisema kuanzia baraza jipya la madiwani, hataki kusikia mchezo huo wa matumizi mabaya ya fedha za serikali kutoka kwa madiwani hao au watumishi.

Mkango alisema amejipanga na timu yake kufuatilia matumizi yote yatakayofanyika na kwamba akibaini matumizi yoyote yatakayofanyika bila kufuata utaratibu, ofisi yake haitasita kuchukua hatua za kisheria kwa wahusika wote.

"Wote kwa pamoja tuwe wazalendo, tumuunge mkono Rais wetu (John Magufuli) ambaye wakati wote amekuwa mstari wa mbele katika kupinga vitendo vya kifisadi," alisisitiza.

# Majaliwa apigia debe matumizi TEHAMA

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ametoa wito kwa wananchi kutumia vizuri Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwenye shughuli za uzalishaji mali na utoaji huduma katika sekta mbalimbali.

Amesema hatua hiyo itasaidia kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini pamoja na kuongeza ajira.

Majaliwa aliyasema hayo juzi katika hafla ya utoaji tuzo kwa washindi mashindano ya TEHAMA yaliyoandaliwa na kampuni ya Huawei na Tanzania kushika nafasi ya pili kidunia na ya kwanza kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Waziri Mkuu alitumia fursa hiyo kuwapongeza washindi na waandaaji wa mashindano hayo. Hafla hiyo ilifanyika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Alisema serikali imedhamiria kufikisha miundombinu ya mkongo wa taifa wa mawasiliano kwenye maeneo mengi zaidi kwa lengo la kuongeza matumizi ya mawasiliano ya kasi (broadband) kutoka asilimia 45 ya sasa hadi asilimia 80 ifikapo mwaka 2025.

Majaliwa alisema ili kufikia malengo hayo, serikali itatoa kipaumbele kwenye masuala ya utafiti na ubunifu sambamba na kutambua na kusajili wataalamu wote wa TEHAMA nchini.

"Vilevile tutaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwamo Huawei katika kuhakikisha tunaanzisha vituo vya umahiri vya sayansi na teknolojia kwenye taasisi za elimu ya juu nchini kwa kuzingatia maeneo ya kimkakati katika kujenga uchumi imara na endelevu sambamba na kudhibiti athari hasi zinazoweza kutokea kutokana na matumizi ya TEHAMA," alisema.

Wakati akizindua Bunge la 12 jijini Dodoma, Novemba 13, mwaka huu, Rais John Magufuli alisisitiza kuwa katika kipindi hiki ambacho dunia iko kwenye mageuzi ya viwanda yanayoongozwa na sekta ya mawasiliano, Tanzania haina budi kuendana na kasi ya kukua kwa sekta hiyo.

Pia Waziri Mkuu alizitaka kampuni za ndani zinajishughulisha na masuala ya TEHAMA ziige mfano wa Huawei kwa kuwekeza zaidi kwa kundi la vijana kwa nia ya kuibua na kuendelea vipaji.

"Serikali kwa upande wake, itaendelea kutekeleza maelekezo ya ilani ya uchaguzi ya CCM kwa mwaka 2020 ya kuimarisha na kuhamasisha matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu katika uchumi wa kidijitali. Maeneo yatakayolengwa ni pamoja na serikali mtandao, miundombinu ya TEHAMA katika nyanja zote za uchumi sambamba na kuimarisha ulinzi wa mitandao," alisisitiza.




Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Khamis Hamza Chilo, akiongozana na Kamishna wa Uhamiaji Zanzibar, Johari Sururu (kushoto), baada ya kumaliza ziara ya ukaguzi wa huduma za kiuhamiaji katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, Visiwani Zanzibar. **PICHA: MAMBO YA NDANI**

# Waitara: Serikali itashirikiana na wanaofuata sheria tu

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mwita Waitara, amesema serikali iko tayari kutoa ushirikiano kwa wenye viwanda ambao wanafuata sheria.

Vilevile, amesema serikali itaendelea kuwajengea mazingira mazuri ya shughuli wawekezaji hao hasa wanapozingatia Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004.

Waitara aliitoa kauli hiyo jan,a alipotembelea na kukagua kiwanda cha Saji Packaging LTD kinachojishughulisha na uzalishaji wa vifungashio vya plastiki pamoja na kurejeleza taka za plastiki kilichoko wilayani Ilemela jijini Mwanza.

Akionyesha kuridhishwa na shughuli za kiwanda hicho, Waitara alisema kimekuwa rafiki kwa mazingira kutokana na kukusanya taka za plastiki ambazo zingezagaa ovyo mitaani, lakini kiwanda hicho huzitumia kama malighafi.

"Kazi ya serikali ni kuhakikisha mnazingatia kanuni, sheria, taratibu na miongozo mbalimbali na mkifanya hivyo, wala hatutagombana na tumekuja hapa tumeona mnafanya kazi vizuri bila kuathiri mazingira na pia mnatoa ajira, watu wanaokota chupa wanaleta hapa, wanapata chochote," alipongeza. Waitara aliwataka wamiliki wengine wa viwanda kufuata utaratibu na sheria ili kuisadia serikali na wanapokwama katika shughuli zao, wasisite kuomba ushauri kutoka mamlaka husika zikiwamo Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Mkaguzi wa TBS Kanda ya Ziwa, Nelson Mugema, aliyefuatana na Waitara katika ziara hiyo, alitoa wito kwa wenye viwanda wengine nchini, kuchukua hatua ya kuthibitisha ubora wa bidhaa katika shirika hilo.

Mugema alisema TBS imeandaa viwango mbalimbali katika vifungashio vya vyakula na bidhaa nyingine ikiwamo mikate.

Aliwataka wafuate utaratibu kwa kupeleka maombi ili vifungashio wanavyozalisha, vithibitishwe ubora kabla ya kupelekwa sokoni ili kumlinda mlaji na mazingira.

Mkurugenzi wa kiwanda hicho, Salim Khahi, aliishukuru serikali kupitia watendaji wake ambao wamekuwa wakimpa maelekezo na ushauri katika kuhifadhi mazingira.

"Hapa katika kiwanda hiki mazingira yanalindwa vizuri na hakizalishi uchafu wa aina yoyote, kila taka za plastiki tunazikusanya hapa na kuzifanyia 'recycling' (kurejeleza)," alisema.

Juni Mosi mwaka huu, serikali ilipiga marufuku matumizi, usafirishaji na uzalishaji wa mifuko ya plastiki ili kulinda mazingira.

Ziara ya Waitara katika mikoa ya Kanda Ziwa akiambatana na watendaji wa NEMC, inalenga kukagua uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 na kuelimisha umma kuhusu juhudi za Serikali katika kulinda mazingira.

# Huduma za kibenki sasa kwa WhatsApp

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhakikisha wateja wanazifikia huduma za kibenki kwa urahisi zaidi, Benki ya I&M imezindua huduma mpya ijulikanayo kama 'Rafiki ChatBanking' inayomwezesha mteja kupata huduma kwa njia ya WhatsApp kwenye simu yake ya mkononi.

Kupitia huduma hiyo, benki hiyo inaendelea kudhihirisha azma yake ya kuendelea kuwa karibu zaidi na wateja kwa kubuni bidhaa na huduma bora ambazo zinampa mteja uhuru wa kifedha na kuboresha maisha.

Akizungumza wakati wa hafla ya uzinduzi wa huduma hiyo juzi, Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Baseer Mohammed, alisema huduma ya Rafiki ChatBanking ni ya aina yake ambayo inasogeza huduma za kibenki karibu zaidi na wateja.

Mohammed alisema huduma hiyo itasaidia kupunguza adha ya kufuata huduma umbali mrefu kwa kuwa inampa mteja uhuru wa kufanya miamala kwa WhatsApp.

"Benki yetu imekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha inaleta huduma na bidhaa za kibunifu ambazo zinafanya maisha ya wateja wetu kuwa rahisi na bora zaidi kwa kutumia fursa mbalimbali ambazo zinaletwa na teknolojia za kidijitali," alisema.

"Tunayofuraha kuitambulisha huduma ya Rafiki Chat Banking kwa wateja wetu. Huduma hii inampa mteja uhuru wa kupata huduma za kibenki mahali popote alipo kwa njia ya WhatsApp, hivyo kudhihirisha azma yetu isemayo 'Tuko Upande Wako'," aliongeza.

Mkuu wa Idara ya Wateja wa Rejareja wa Benki ya I&M, Lilian Mtali, alisema huduma hiyo ni salama na rahisi kutumia inayomruhusu mteja kupata huduma za kibenki zikiwamo kutuma pesa ndani na nje ya benki, kuangalia salio, kulipia bili mbalimbali pamoja huduma za kuhamisha pesa kutoka au kwenda kwenye mitandao ya simbanking.

"Tunatambua kuwa si kila wakati wateja wanapata muda wa kutembelea benki au ATM, ili kupata huduma kutokana na kuwa na majukumu ndiyo maana tumekuja na Rafiki ChatBanking ambayo inamruhusu mteja kupata huduma zote za kibenki popote alipo," alisema.



BOSI TALGWU MWANZA:

## Waajiriwa Serikali Mtaa wote mkoani tunao, walitimuliwa 300 tukawarejesha




# BUFE

IJUMAA DESEMBA 25, 2020

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA


Ukurasa 12

## Walimu wawili wanafundisha shule nzima

PROF: OLE GABRIEL

# Katibu Mkuu Mifugo na darasa la ng'ombe wa 'Uchumi wa Kati'

## •DC Musoma adaka na kunadi kwake

**Na Sabato Kasika**

KUFIKA uchumi wa kati, maana yake Tanzania imeingia uchumi wa viwanda. Wafugaji wanakumbushwa kuacha kufuga kienyeji, sasa wahamie stadi za kisasa kupata mazao yenye ubora kwa matumizi ya viwandani.

Ni ufugaji upi? Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Elisante Ole Gabriel, anautaja ni kuhimilisha mifugo kupata maziwa mengi, nyama nyingi na ngozi bora kwa ajili ya viwandani.

"Wafugaji wanatakiwa kufuga kisasa, kwa ajili ya kuwaongezea kipato, kwa kutumia teknolojia ya uhimilishaji, ambayo inayomwezesha mfugaji kuchagua mbegu bora ya ng'ombe mwenye uwezo wa kutoa maziwa mengi," anaeleza.

Profesa Ole Gabriel, anasema teknolojia ya uhimilishaji, inaruhusu ng'ombe kupandikizwa bila dume na kupata mbegu bora ya ng'ombe anayeweza kutoa lita 20 hadi 30 za maziwa kwa siku.

Anatoa somo hilo katika utambuzi wa ng'ombe wa Kata ya Bugwema wilayani Musoma mkoani Mara na kwamba uhimilishaji pia unamwezesha mfugaji kuchagua aina ya anayemtaka na jinsia ya ng'ombe anayotaka.

"Teknolojia ya uhimilishaji pekee, ndio inayoweza kumfanya mfugaji kupata rasilimali za kuendesha viwanda vinavyotengeneza bidhaa zitokanazo na maziwa ama ngozi," anasema Profesa Ole Gabriel.

Katibu Mkuu huyo, mtaaluma wa masoko anashauri umma kubadili mtazamo wa kufuga kibiashara, kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya uhimilishaji, ambayo ni mkombozi na tayari imeshaleta mapinduzi makubwa kwa wafugaji nchini.

Katibu Mkuu huyo anafafanua kwa mfano wa mfugaji mwenye ng'ombe bora wanaompatia wastani wa lita 20 kwa siku, inamwongezea kipato maradufu.

"Pia, mfugaji atakuwa na uhakika wa kupata nyama na ngozi bora baada ya ng'ombe wake atakapofikisha umri wa kukoma kuzaa, hivyo mtindo kuwa na kundi kubwa la ng'ombe umepitwa na wakati," anasema.

Anaitetea mifugo kuwa ni utajiri na wafugaji wanatakiwa kuwa tayari kutoa ushirikiano kwa wizara yake, ili kuanzisha mradi wa ufugaji wa kisasa wenye ng'ombe bora katika kata hiyo ya Bugwema na wilaya kwa ujumla.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Elisante Ole Gabriel. **PICHA: MTANDAO**

Rai yake kwa Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Vincent Anney, madiwani na wasaidizi timu ya mbunge kuelimisha wafugaji umuhimu wa uhimilishaji.

**DC MUSOMA**

Dk. Vincent Anney anasema, anaahidi kuwatuma wasaidizi wake katika kata mbalimbali za wilaya, kutoa elimu kuhusu uhimilishaji ili kufanikisha kazi hiyo.

"Uhimilishaji unaweza kuwa mgeni kwa wafugaji wengi, hivyo ni muhimu kuwapa elimu waelewe, ili iwe rahisi kukubali teknolojia hiyo yenye manufaa makubwa kwao," anasema mkuu wa wilaya.

Anaendelea kwamba, kuna wafugaji wanaofurahi milki ya makundi makubwa ya ng'ombe, hivyo ni muhimu kuelimishwa wabadilike, akitoa mfano wanalazimika kuhama kila msimu kutafuta maji na malisho na hata wanaangukia migogoro kati yao na wakulima.

"Ninaamini kwamba, wafugaji wote wakizingatia maelekezo ya wizara na kutumia teknolojia ya uhimilishaji, watapata faida kubwa kuliko kuendelea kuzunguka na ng'ombe wengi wenye faida ndogo," anasema.

Inaelezwa Tanzania ilipopata uhuru mwaka 1961, ilikuwa na ng'ombe milioni tisa, lakini sasa wameongezeka hadi milioni 30.5, huku idadi ya watu nayo ikiongezeka kutoka milioni 10 ya wakati huo hadi milioni 55 wa sasa.

Kwa mujibu wa Rais Dk. John Magufuli, katika moja ya mikutano yake ya hadhara, alitamka: ""Mifugo inaongezeka, watu wanaongezeka, shughuli zikiwamo za kilimo nazo zinaongezeka.

"Suala la ng'ombe 5,000 tano unakuwa unazunguka nao limepitwa na wakati. Sisemi mpunguze idadi ya ng'ombe, isipokuwa niwaombe wachungaji tuanze kufuga kisasa," anasema.

Rais anawataka wenye ng'ombe wengi, wahamie kufuga wachache na ziada wajenge hata nyumba za kisasa, kuchimba bwawa kubwa la maji kwa ajili ya mifugo yake, akikumbusha Tanzania iko katika vinara bora kuwa na ng'ombe wengi, ikiongozwa na Ethiopia.

UCHUMI

## MTIHANI WA AJIRA....

# Walimu wawili wanafundisha shule nzima

- Kusimama mwanzo mwisho...nyumbani hoi!
- Vyumba 3, wanavyojigawanya kitendawili
- Ufaulu palepale; uhalali wa shule mgogoro

**Na Beatrice Shayo, aliyekuwa MBARALI**

"HAPA nina matatizo yananisumbua kwa muda mrefu, natakiwa kufundisha vipindi 25, kwa wiki vinafika zaidi ya 97. Unaweza kuvuta picha ninafanya kazi katika mazingira gani," ni maneno ya Mwalimu Msaidizi wa Shule ya Msingi Iyala, Filbert Mhagama (35).

Anasema ni hali inayomwacha katika mazingira magumu ya kazi ya ufundishaji katika shule hiyo iliyoko kijijini Iyala, Kata ya Luhanga, wilayani Mbarali, mkoani Mbeya.

Kwa mujibu wa Mwalimu Mhagama, shule ilianzishwa mwaka 2015 akiwa mwalimu pekee na mzizi wa wanafunzi waasisi watatu kutoka shule mama ya Iyala. Muda mfupi baadaye, waliongezeka hadi 72 na sasa jumla yao wako wanafunzi 244, ikifika darasa la sita.

Mhagama anayetumika pia wajibu wa mwalimu mkuu, anarejea mwongozo wa elimu unaomtaka mwalimu afundishe darasa lenye wanafunzi wasiozidi 45 na anawasilisha masikitiko, kufanya kazi katika mazingira magumu kutokana na kuwapo walimu wawili pekee.

Mwalimu huyo anadokeza mgawanyiko wa kutumia madarasa matatu yaliyopo, moja linatumiwa na; awali na la kwanza, huku la pili wako katika mbadala wa kuingia mchana.

Pia, anataja darasa la sita wapo 59 na la tano 45. Anafafanua: "Kwa darasa la nne wanakaa wenyewe hatujawachanganya kwa kuwa hawa wanafanya mitihani ya kitaifa, hivyo tukaona wabaki wenyewe wasichanganywe.

"Vipindi vyetu vya ufundishaji kuna wakati darasa moja linakosa vipindi kwa kuwa utanikuta asubuhi nimeingia darasa jingine na hilo darasa wakati huo huo anatakiwa mwalimu aingie kuwafundisha, tunashindwa kujigawa."

### WANAVYOFUNDISHA

Mhagama, mwajiriwa wa mwaka 2009 na kuhamia shule hiyo mwaka 2015 alipopelekwa kuanzisha, ikiwa na madarasa mawili.

Anaeleza mbinu ya kazi yao, pindi anapoingia kwenye darasa lililochanganywa wanafunzi wa makundi mawili, wanafunzi wasiohusika na kipindi, hutakiwa kutulia mpaka wanapomaliza somo husika.

"Nikiingia kwenye kipindi cha darasa la sita, ina maana hawa wanafunzi wa darasa la tano hawatakiwi kufanya chochote wananisikiliza," anasema Mhagama.



Mwalimu Filbert Mhagama kushoto, akiwa kazini kwake. Picha nyingine, Elizabeth Manyanga, mkazi wa Iyala, akifafanua jambo kuhusu adha ya shule hiyo.

> **"Kipindi cha darasa la sita nikishatoka, ataingia mwalimu mwenzangu kama kipindi kinamruhusu kuingia, wakati mwingine utanikuta naunganisha humo humo," anaeleza Mhagama.**

"Kipindi cha darasa la sita nikishatoka, ataingia mwalimu mwenzangu kama kipindi kinamruhusu kuingia, wakati mwingine utanikuta naunganisha humo humo," anaeleza Mhagama.

Pia, anataja shida ya maji inawafanya kwenda kuchota umbali wa kilomita tatu, hata wanachelewa darasani. Hapo Mwalimu Mhagama, ana simulizi: "Wanafunzi wanafuata maji saa 12 asubuhi.

"Inategemea kuna wengine wanatembea umbali wa kilometa 10 kufika shule, ndipo aende kuchota maji mpaka warudi unakuta kipindi kimeanza kwani wanafika saa 2:30 asubuhi."

Anasema, alishawasilisha dai kwa mamlaka na walitengenezewa kisima kilichotumika kwa mwezi mmoja, kisha kiliharibika na hakijatengenezwa tena.

Mhagama anadokeza kwamba: "Tukatafuta mafundi wakaja kutengeneza, tukatumia siku chache kikaharibika."

### MZIGO WA KAZI

Anasema ni kawaida anafika nyumbani hoi, kutokana na mzigo mkubwa aliyo nao shuleni, akianika simulizi hao kwa kauli: "Unaingia darasa hili unatoka, unaingia darasa hili unatoka kila darasa lina zaidi ya wanafunzi 40.

"Yale madarasa tuliyoyachanganya wanazidi 100. Kingine kinachotuchosha zaidi, unajikuta una mzigo mkubwa wa madaftari kusahihisha hapo hapo, tuna mitihani kwa ajili ya darasa la nne.

"Kuna muda tunatakiwa tujitoleea zaidi kwa ajili ya darasa la nne. Sasa ukiwaza kuwaacha inakuwaje? Hawa lazima tuwajengee msingi mzuri!"

Ni mbinu gani mbadala anayochukua? Mwalimu Mhagama anaendelea: "Inabidi tuwatafute wanafunzi wenye uelewa kuandika mitihani wa darasa la nne na sisi tunakuja kuisahihisha ili tuendelee na vipindi katika madarasa mengine.

"Nashindwa kuondoka saa 11 kwa sababu kuna wanafunzi wanaishi umbali wa zaidi ya kilomita 10, sasa mtoto kama huyo ukimruhusu aondoke saa 11:00 jioni atafika nyumbani saa tatu usiku, halafu tena aondoke asubuhi kuja shule atachoka zaidi.

"Hatuna nyumba za walimu, ina maana tunajitegema. Nimepanga chumba na sebule hazina ubora unaotakiwa. Nyumba haina sakafu, imetulazimu kuishi hivyo bado una familia," anasema.

"Shida nyingine ni shule haina usajili, mimi ndiye niliyeianzisha mwaka 2015 nikiwa peke yangu hadi Julai 2017, nikaletewa mwalimu ambaye alidumu kwa miezi mitatu na kustaafu," anasimulia.

Anasema usajili za wanafunzi wa shule anayofundisha iliyoanzishwa pasipo msaada wa serikali hata upanuzi wake, hadi sasa ipo kwenye shule mama ya Iyala inayobeba jukumu la mwalimu mkuu.

### MWALIMU MWENZA

Kama kilivyo kilio cha Mwalimu Mhagama, Titus Cuthbert, anasema idadi ya vipindi vyake ni zaidi ya 15 kwa siku na kwa wiki vinagota 92, ilhali wastani wa vipindi anavyotakiwa kufundisha kwa wiki ni 25.

"Nikifika nyumbani ninakuwa katika hali ya uchovu sana, unasimama zaidi ya saa nane, ukitoka darasa hili unaingia jingine kama ni kupumzika ni dakika chache muda mwingi ni kusimama madarasani," analalamika kutumia muda mrefu kusimama.

Anasema, pindi inatokea mwalimu mwenzake amepata dharura, analazimika kila darasa afundishe kipindi kimoja, ingawaje katika sura ya pili ana kifuta machozi chja mafanikio ya mitihani.

Mwalimu huyo anasema katika matokeo ya wanafunzi darasa la nne, ni watano waliofeli kati ya 60 na mwaka uliofuata, ambao wako darasa la tano hivi sasa, wanafunzi saba walifeli kati ya 51.

### WANAFUNZI WANENA

Mwanafunzi Serafina Hamis (18), anayesoma darasa la sita, anasema huwa anashindwa kuwaelewa walimu, kwani huwa wanafundisha haraka wawahi kuingia madarasa mengine.

Anasema, kwa siku huwa wanasoma vipindi vitatu na wakati mwingine kipindi kimoja, walimu wanapoelemewa na muda wa kuwafundisha.

Serafina anaeleza mazingira magumu pindi wanapochanganywa madarasa, kwamba: "Tunashindwa kuelewa vizuri kwa sababu tunakaa chumba kimoja chenye madarasa mawili. Tunashindwa kufanya kazi za darasani, kwa sababu kuna mwalimu mwingine anaingia kufundisha."

Anasema kuna wakati hawasomi walimu wanaopokuwa kwenye madarasa mengine au wanaambulia kipindi kimoja, akiambatanisha na kuchelewa darasani kunakotokana na kuchota maji mbali.

Shabani Mwasikamile (17) wa darasa la sita, naye ana kilio cha mwenziwe kutokumwelewa mwalimu, kunapotokea anafundisha haraka awahi kwenye darasa lingine.

"Kuna wakati mwalimu amepata dhararu na shule amebaki mwalimu mmoja, ujue tunaweza kusoma kipindi kimoja ama tusisome kwa kuwa mwalimu mmoja anatingwa na vipindi vingi," anasema Shabani.

Anataja tatizo jingine ni wanafunzi darasa la kwanza, la pili na awali wanakaa chini kwa kukosa madawati.

### WAZAZI & MAJIRANI

Mjumbe wa Halmashauri ya Kijiji cha Iyala, Bonifance Ndunguru, anasema wamejitolea kuongeza madarasa katika shule hiyo baada ya kubaini wanafunzi wanataabika.

Anasema serikali iliwapa ramani kuanza kujenga majengo ya shule hiyo, lakini katika mazingira tatanishi wamezuiliwa kuendekeza mradi huo.

"Hatuelewi tatizo ni serikali au kuna wengine! Maana serikali ilitoa vibali vya ramani, leo hii wanatuzuia tusijenge wakati wananchi tumejitolea kwa fedha zetu kujenga hii shule hadi ilipofika," anaeleza Nduguru kwa mshangao.

Elizabeth Manyanga, mkazi wa Iyala, anasema walipewa ridhaa kujenga shule hiyo, kiasha ghafla kukaja zuio kutoka uongozi wa wilaya, kuhusu uendelezazo ardhi hiyo katika shule iliyofikia darasa la sita, wakiagizwa "ni ardhi ya mwekezaji tangu mwaka 1970."

"Hatujapewa waraka wowote, serikali inasema elimu kwanza tumejenga shule ili watoto wasome, lakini tunanyanyasika kwa kuzuiliwa na ujenzi hapa tunaendelea na ujenzi kwa siri licha ya kutuzuia," anasema Manyanga.

### MKUU WA WILAYA

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, anasema alizuia ujenzi shuleni hapo kwa muda na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, angeenda kutolea ufafanuzi.

"Ni kweli nimezuia ujenzi na Mkuu wa Mkoa atakwenda kulitolea ufafanuzi kwa kuwa ni huduma kwa jamii niliwaambia wasimame kwa muda," anasema.

Mfune anarejea sheria inazuia kujenga ndani ya hati ya mtu mwingine, huku akifafanua huduma zinazotolewa shuleni hapo haziridhishi, madarsa yako machache, wanafunzi wengi na wanaendelea kuongezeka.


"Kama shule ina walimu wawili, ina maana hairidhishi kwa sababu huwezi ukawa na shule ikawa na walimu wawili watoto wakasoma vizuri," anasema.



Wanafunzi wa madarasa mawili tofauti katika Shule ya Msingi Iyala, wakiwa darasani. **PICHA ZOTE: BEATRICE SHAYO**

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Wananchi fuatilieni ahadi za washindi






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
jkulangwa@yahoo.com

WATANZANIA ni miongoni mwa viumbe wa Mungu waliojaliwa usahaulifu mkubwa sana. Ni watu rahimu ambao leo utawaambia hili na usiku ukiingia, kesho wataamka na mapya kabisa.

Tumemaliza uchaguzi mkuu na viongozi wamepatikana. Waliofurahi na kukenua meno wamefanya hivyo na waliosikitika na kununa nao wamepata fursa yao, ili mradi hatuwezi kulingana na kufanana kifikra na kihisia.

Tumeshuhudia waliofurahi kwa kupata ushindi wa kishindo na kulaumu wanaochukia na kusema uchaguzi haukuwa huru na wa haki. Lakini, tumewaona waliokunja midomo na sura na kusema kilichofanyia kaniwizi na ulaghai. Kila mwamba ngoma, lazima ngozi aivutie kwake.

Kabla ya upigaji kura wa Oktoba 28, kulikuwa na miezi mitatu ya kampeni, zilikuwa kampeni zilizogubikwa na ahadi kedekede, maneno matamu ya kuvutia kura na mengine machungu ya kupondana.

Kila mgombea alitaka achaguliwe, ili aongoze au kuwakilisha wananchi kwa kipindi cha kwanza cha miaka mitano au cha pili cha miaka mitano na akijitapa kumaliza matatizo ya watu na kuleta maendeleo katika eneo lake au nchini.

Pili, kazi zilizokuwapo wakati wa kampeni hazionekani tena, licha ya mabango yaliyopauka kuendelea kuning'inia kwenye miti na kutazama jengo mitaani, ambayo ndiyo yanayorejesha kumbukumbu za uchaguzi miongoni mwetu.

Simulizi zilizoko mitaani ni nani alifanya nini, nani alisema nini na msanii gani alitia fora katika kampeni za kumnadi mgombea fulani? Lakini, wapo wanaojadili nani alivuna nini katika kinyang'anyiro hicho na nani alikula hasara.

Sio siri, wapo waliouza mali zao ili kupata fedha za kugharamia uchaguzi kwa matumizi ya mizunguko, kununua wapiga kura na kulipa wasanii au vikundi vya kampeni. Waliokosa kuchaguliwa ndio wanaolia na kusaga meno.

Lakini, wapo wanaojipongeza na kupongezana kwa kufanya shajara za hapa na pale, wakijua wazi kuwa si siri, ushindi walioupata ni kuyashinda maisha kwa kuwa mwishowe ni kipato na uhakika wa kuishi.

Hakuna asiyejua kuwa uchaguzi nchini ni uhakika wa maisha mazuri, kwamba kuchaguliwa ni kuukata na ni fursa ambayo hakuna anayekubali kuikosa kirahisi rahisi tu. Ndiyo maana nguvu kubwa na mbinu kali hutumika.

Ingawa Rais John Magufuli kila mara amekuwa akiwaasa wateule wake, kwamba ukichaguliwa usisherehekee kwa sababu unaweza usidumu katika nafasi yako, kwa kuwa hakuna uhakika wa kudumu, lakini kwa wateule si uhalisia.

Watu wakishateuliwa, hujua dhahiri kuwa umasikini wameuagana kukaribisha ukwasi na uheshimiwa ambao unawatenganisha wanyonge na wenye nguvu, lakini hadharani wataigiza utii kwa mteuzi wao, huku wakifurahia nyoyoni.

Hapo ndipo Watanzania nao wakishawapata viongozi wao, hujisahau na kurejea katika maisha ya kawaida na kuacha kufuatilia walichoahidiwa, wakati wa kampeni na kubaki kuwasifia na kuwashangilia kwa kila walisemalo.

Pengine ingefaa, mbali na ilani za uchaguzi za vyama hata wagombea kwa ngazi za majimbo na kata, wakawa na ilani zao ndogo zinazohusu maeneo yao ili baada ya kuchaguliwa wananchi wafuatilie na kuwatathmini.

Mathalan, kuna mahali mgombea ubunge ambaye ameshinda, aliahidi kuwapelekea wananchi wake mabasi ya mwendokasi, huku akijua fika kwamba jimboni mwake si rahisi kuwa na barabara za mabasi hayo, achilia mbali kujua tu kwamba mradi huo ni wa kitaifa.

Je, hivi sasa mwakilishi huyo wa wananchi akiulizwa miundombinu ya mabasi hayo ataipitisha wapi, atakuwa kweli katika nafasi ya kuelezea atakavyoijenga na kuhakikisha mabasi hayo yanapatikana kweli?

Baada ya uchaguzi huwa ni kila mtu kuangalia maslahi yake binafsi na kusahau kuwa kwenye kampeni alitoa kauli ambazo kumbe bila kujua au kwa mihemuko ya kisiasa, zilikuwa juu ya uwezo wake na sasa kuwa vigumu kuzitekeleza.

Kama wananchi wamesahau walichoahidiwa na wagombea wakati huo wa kampeni, basi hivi sasa wasikose kuhudhuria mikutano yao na kuwataka warejee kauli zao za wakati wa kampeni, zilizokuwa zimesheheni ahadi kedekede za kuwabadilishia maisha yao. Alamsiki!

UCHUMI

BOSI TALGWU MWANZA:

# Waajiriwa Serikali Mtaa wote mkoani tunao, walitimuliwa 300 tukawarejesha

- Atamba kufika kona zote kwa TEHAMA
- Bando za simu, pensheni kwa wastaafu

**Na Anthony Gervas,**

**MWANZA**

**BAADA ya kunufaika na simulizi za kazi za jumuiya ya wafanyakazi mkoani Mwanza -TUGHE katika safu ya jarida hili hivi karibuni, pata mwendelezo wa simulizi za mwandishi kuhusu kinachofanyika kutoka chama kingine mkoani humo, TALGWU, fuatilia:**



Katibu wa TALGWU Mkoa wa Mwanza, Audax Stephano. **PICHA: ANTHONY GERVAS**

NI Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa nchini kinachotetea kulinda haki za wafanyakazi kazini, mahsusi watumishi wote wa serikali za mitaa, isipokuwa walioko sekta ya elimu kushikamana na Chama cha Walimu Tanzania (CWT).

Pia, wapo wafanyakazi waliokuwa kwenye serikali za mitaa na baadaye wakahamishiwa serikali kuu mikoani kwa uhamisho wa kawaida, kama hospitali za mikoa na kanda na mashirika ya dini, nao wanaelezwa uanachama wao unaendelea.

Katibu wa TALGWU Mkoa Mwanza, Audax Stephano, ana ufafanuzi kuhusu chama hicho kwamba ni: "Majukumu yetu (TALGWU), hususani mkoa wa Mwanza tunalinda na kutetea haki za wafanyakazi.'

Anaorodhesha wadau wanachama wakuu ni kutoka halmashauri mbalimbali za miji, jiji, manispaa na wilaya, huku akifafanua utaratibu uliopo, wahusika wasijiunge na vyama viwili kwa wakati mmoja.

Stephano anaeleza mazingira wanakojitosa kutoa utetezi ni pale mfanyakazi anadai haki kisheria, hakijihisi kuonewa, chama humwakilisha mfanyakazi kwa mwajiri kumtetea haki zake za msingi.

Anasema mwaka 2018 wafanyakazi 300, wengi wakiwa watendaji wa vijiji na kata kutoka mkoani Mwanza, kati ya 8,000 waliokosa sifa ya kidato cha nne, waliondolewa kazini, TALGWU iliwatetea na walirudishwa kazini.

Stephano anasema, hatua hiyo ilitokana na waraka wa serikali wa mwaka 2004, uliotaka baada ya mwezi Mei ya mwaka huo, waajiriwa kuwa na vyeti vya kidato cha nne, lakini wafanyakazi waliajiriwa kabla.

Anasema baada kubaini waajiriwa hao hawakuwa na makosa, chama kiliwasilisha hoja za msingi serikalini kuhakikisha watumishi wanapata haki zao za kurudishwa kazini.

Anasema wafanyakazi ambao waliondolewa kazini ni waliokuwa wameajiriwa baada ya waraka wa sheria kupitishwa akinukuu "mfanyakazi atakayeajiriwa tena kazini awe na cheti cha kidato cha nne", hivyo wana wajibu wa kuhakikisha haki na stahiki za wafanyakazi zinalindwa.

Anataja mengine, ni pamoja na kusimamia uwepo wa usalama kazini, mfano wafanyakazi walioko katika Kitengo cha Ukimwi na Kifua Kikuu (TB) na watumishi wa afya visiwani, wote wanakabiliwa na mazingira hatarishi kikazi kuambukizwa maradhi.

Katibu huyo anataja adha ya wafanyakazi kufukuzwa au kisingiziwa, akisema chama huwa kinawajibika kulipeleka mahakamani kupigania kwa kutumia mawakili wake wanaoshirikiana na maofisa wa TALGWU.

Huku akiahidi kuwekwa mabaraza ya wafanyakazi sehemu za kazi, kwani ni chombo anachokieleza ni muhimu katika ushirikishaji wafanyakazi katika sehemu zoa za ajira.

"Mwanza, tutahakikisha kuna mabaraza hai ya wafanyakazi kwenye wilaya zote nane, ili kutetea na kulinda haki na stahilki zao kazini," anasema.

Kimsingi Baraza la Wafanyakazi, lilianzishwa mwaka 1971 kwa mwongozo wa chama- TANU katika zama hizo za chama kimoja cha siasa na kutekelezwa kiserikali, lengo ni kufungua fursa ya haki ya mfanyakazi kazini.

Anafafanua TALGWU imeanzishwa na kusajiliwa rasmi mwaka 2001, sambamba na Chama cha Wafanyakazi wa Serikali Kuu na Afya (TUGHE).

**MAFANIKIO YALIVYO**

Stephano anataja mafanikio ya kudumu ni kwa wanachama wanaoshirikishwa vikaoni na wawakilishi wake ngazi ya matawi hadi taifa, wanachama kitaifa wanaongezeka kutoka 3,000 hadi kufikia 5,000 hivi sasa.

Pia, kwa Mkoa Mwanza, anajivuna kupigwa hatua ya kuwapo mfumo wa mtandao wa wanachama unaosaidia kujua taarifa, waliko na kama wana matatizo, ili waingilie kati suala hilo baada ya kuwasiliana nao.

Anadokeza hadi sasa matawi ya uwakilishi waliopo nao kitaifa yameongezeka kutoka 41 hadi 52 na katika mtandao wa simu, kuna matarajio ya kufugua bando ili wadau wahamasisike kujiunga, wakilenga 7,000 kutoka 5,000 wa sasa.

Stephano anaongeza lingine lililoko jikoni, kuanzisha 'kliniki' maalum ya kuwatembelea na kuwafikia wanachama walipo, ili kusikia shida zao na kuzitatua hapo hapo.

Lingine analitaja, ni kutanua mazingira ya ufanyaji vikao na wakurugenzi wa halmashauri mbalimbali, maofisa utumishi na Katibu tawala wa Mkoa (RAS) Mwanzo, ili kupata taarifa zao za mrejesho wa kazi. Vivyo hivyo, wanajipanga kuchagua viongozi.

Stephano anaeleza kwamba, TALGWU Mwanza imeamua kuanzisha programu ya kusajili Chama cha Kuweka na Kukopa (SACCOS), kwa manufaa ya wfanyakazi wanachama, wigo wa chama, ikitarajiwa kuanza ndani ya miaka minne ijayo.

Anaeleza, mwanachama anapostaafu hupewa mtaji wa kuku 20 wa kutaga mayai na jogoo watatu, kumuinua katika maisha mapya anayoanza.

Eneo lingine analolitaja ni kutembelea wanachama wafiwa na kushirikiana nao katika majonzi.

**VIKWAZO VYAO?**

Stephano anataja magumu yanayowakabili ndani ya chama ni pamoja na mwingiliano wa wanachama wao na chama cha TUGHE, katika maeneo ya Idara ya Afya ambao ina wanachama kutoka Hospitali za Rufani, Kanda na mashirika ya dini.

Anatoa mfano mkoani ni katika Hospitali za Sekou-Toure na Bugando, ambao zina wafanyakazi wa serikali kuu, lakini kati yao wapo wa chama TUGHE, jambo linaloleta mgogoro kati ya vyama hivyo viwili.

Anasema msamiati 'afya' katika pande zote za vyama, ndiyo kikwazo kinachovuruga mipaka ya wanachama na kusababisha mwingiliano anoutaja katika wilaya za Sengerema na Misungwi.

Katibu huyo wa TALGWU ana ufafanuzi kwamba: "Sisi serikali mitaa, wafanyakazi wetu ni wale walioko kwenye zahanati, vituo vya afya, miji, jiji na hospitali za wilaya."

**NINI UTATUZI WAKE?**

Katibu Stephano anaifafanulia Nipashe kwamba, kisheria inapotokea chama kimoja kuingiliana na kingine, vyote vinatakiwa kwenda na shauri katika Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (TMA).

Aidha, anataja kuwapo waraka wa kutatua migogoro na mipaka ya vyama chini ya Wizara ya Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu.

Stephano anataja kutokea mgongano wa sheria za kazi, akiwaelekezea lawana waajiri wasiotambua na kuheshimu sheria na matakwa yake kimataifa, kwamba kuwa vipo kwa ajili ya maslahi mapana ya wafanyakazi na umma.

Pia, anazungumzia haki wanazozipigania kila kukicha hazitekelezwi kwa wakati na kuna wafanyakazi wanaoidai serikali madeni mishahara haki nyinginezo kama fedha za kujikimu na likizo kama wanazodai walimu.

"Katika mkoa wa Mwanza, serikali inadaiwa madeni ya zaidi ya shilingi bilioni tatu, ikiwamo deni la shilingi milioni 200 la Wilaya ya Buchosa, baada ya kumeguka kutoka Wilaya ya Sengerema," anaeleza Stephano.

Pia, anataja dai la wafanyakazi kutokupandishwa vyeo na madaraja yao tangu mwaka jana hadi sasa,

kuelekea 2021 hakuna waliopandishwa, akitoa shaka ni ucheleweshwaji unaokwaza uchapa kazi.



Watumishi wa Serikali ya Mtaa, wadau wa TALGWU wakiwajibika katika Duka la Dawa la Hospitali ya Wilaya ya Magu. **PICHA: MTANDAO.**





Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani (wa pili kushoto mbele), akizungumza na watendaji wakuu wa Shirika la Umeme (TANESCO) alipotembelea kwenye mradi wa kituo cha kufua umeme kilichopo Zuzu Dodoma jana, (kulia) msimamizi mkuu wa miradi ya umeme Peter Kigadiye. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Waziri awahakikishia umeme wawekezaji

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amewataka wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza nchini kutokana na uwapo wa umeme wa uhakika kwa wakati wote.

Dk. Kalemani alitoa wito huo juzi wakati alipotembelea kituo cha kufua umeme kilichopo Zuzu jijini Dodoma, baada ya kukamilika kwa asilimia 100. Kituo hicho kinatarajia kuzalisha umeme wa kilovoti 220.

"Kutokana na hatua ya kukamilika haraka kwa mradi huu, nitoe wito sasa kwa wawekezaji kuja kuwekeza mkoani hapa ambapo ni makao makuu ya serikali," alisema.

Kalemani alisema serikali imetoa dola za Kimarekani milioni 24 kwa ajili ya utekelezaji wa kufufua umeme kwenye kituo hicho.

Alisema ametumia nafasi hiyo ili kujihakikishia kama fedha zilizotolewa na serikali zimetekeleza kwa ufanisi mradi huo ambao umefanyika kwa haraka na Watanzania watapata umeme wa kuaminika wakati wote.

Hivi sasa, alisema, Dodoma kuna umeme wa kutosha ambao ni mkubwa unaoweza kujitosheleza kwa watumiaji wa nishati hiyo, hivyo akawaomba wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza kwa muda wote.

Waziri huyo pia aliwapiga marufuku mameneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) katika kipindi hiki cha sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya kukata umeme na kusisitiza uwake kwa muda wote wa saa 24.

Alisema kutokana na kuwapo kwa umeme huo wa kutosha, anawaagiza mameneja wote kote nchini, kutokata umeme na atakayethubutu kufanya hivyo atachukuliwa hatua.

"Watanzania wanataka kufanya mambo yao. Hii ni hata baada ya sikukuu hizi kupita, hivyo hakuna sababu ya kuwakatia umeme wananchi," alisema.

Waziri huyo aliwataka mameneja wote wa wilya na mikoa kuhakikisha kuwa wanawaunganishia huduma ya umeme wananchi wote ambao wameshalipia huduma hiyo kwa wakati.

# Watakiwa kuhuisha leseni kabla ya Des. 31

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WAFAMASIA, mafundi dawa sanifu na wasaidizi wamekumbushwa kuhuisha leseni zao kabla ya Desemba 31, mwaka huu, ili waendelee kufanya kazi za kitaaluma kwa mwaka unaokuja.

Msajili wa Baraza la Famasi Tanzania, Elizabeth Shekalaghe, alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, jijini hapa.

Shekalaghe alisema kwa mujibu wa kifungu namba 22 cha Sheria ya Famasi, Sura 311 wafamasia wanatakiwa kuhuisha majina yao kwenye rejista kwa utaratibu maalamu.

"Pamoja na Baraza la Famasi kuwasajili wanataaluma kwa mujibu wa kifungu cha Sheria ya Famasi nchini, kifungu kinatutaka kabla ya Desemba 31 ya kila mwaka kuhuisha majina ili kufanya kazi za kitaalam kwa mwaka unaokuja,"alisisitiza.

Sambamba na hilo, Shekalaghe alikemea uuzaji wa dawa holela huku akisema limekuwa sugu nchini.

"Mwaka huu Waziri wa Afya (Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto) ameidhinisha kanuni za udhibiti na usimamizi wa uuzaji wa dawa za cheti, hivyo amewataka wanataaluma wa famasi kuhakikisha wanazisoma na kuzielewa kanuni hizo," alisema.

"Kama wafamasia na wataalam tukumbuke tuna watu tunawasimamia na kuhakikisha dawa tunazitoa kwa kuzingatia miongozo iliyopo na baraza halitasita kumchukulia hatua yeyote atakayeenda kinyume cha kanuni hizo," aliongeza.

Shekalaghe pia aliwataka wananchi kutoa taarifa kwenye baraza hilo pale wasiporidhika na huduma zitolewazo katika famasi na maduka ya dawa muhimu nchini.

"Kama mtu atakuwa na dukuduku lolote kuhusu huduma zitolewazo na famasi na maduka ya dawa, anaweza kupiga simu namba 0736 222 504 au namba bila malipo 0800110015 ili kutatua changamoto wanazozipata wakati wanapatiwa huduma hizo," alisema.

# Mbunge ataka mafundi ujenzi kuwa na umoja

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MBUNGE wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, amewataka mafundi ujenzi kuwa na umoja ili kutambulika na kunufaika na fursa za ujenzi zilizopo jijini Dodoma.

Mavunde aliyasema hayo jijini hapa juzi katika halfa iliyoandaliwa na kampuni ya uuzaji wa vifaa vya ujenzi ya Najel na kuwakutanisha zaidi ya mafundi ujenzi50.

Alisema umoja huo utasaidia kundi hilo kuunganishwa na fursa za ujenzi zinazopatikana jijini hapa ili kunufaika na uwapo wa makao makuu ya nchi.

Mavunde alisema baada ya kujiunga au kuunda umoja huo, watanufaika, kwanza kwa kuwa na anwani lakini pia kupata fursa mbalimbali za kutoa huduma ya ujenzi.

"Mkiwa na umoja wenu, zinapotokea kazi inakuwa rahisi kuwaunganisha. Unawaambia tu kuwa nenda sehemu fulani utapata mafundi wazuri, waaminifu ambao watafanyaka kazi nzuri. Hii itasaidia hata mmoja wenu akifanya jambo la tofauti awe anapoteza sifa ili asiwachafue wengine," alisema.

Mavunde alisema pamoja na kuwa na mafundi wengi jijini hapa, kikubwa ni uaminifu ambayo ni silaha ya mafanikio.

Alisema wako watu hawana mtaji wa fedha lakini wana mtaji wa uaminifu, hivyo kupitia uaminifu huo wamekuwa wakipata kazi nyingi na kusisitiza kuwa kupitia umoja huo, atawasaidia mafundi hao kupata bima ya afya ili kuwa na uhakikia wa matibabu.

"Kwa kazi ambazo mnazifanya ni lazima muwe na bima ya afya. Ni lazima tuilinde nguvu kazi yetu. Na katika hili siku yoyote mkiwa tayari niambieni nitawatafutia mtaalam aje awaelimishe kuhusu masuala ya bima ya afya sambamba na umuhimu wake," alisema.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Najel Builders, Neema Nzwalile, alisema kutokana na changamoto ya wajenzi wengi Dodoma kukosa mafundi na ushauri wa kitaalamu kampuni hiyo iliamua kutafuta suluhisho la tatizo hilo.

Nzwalile alisema waliamua kumrahisishia mjenzi kupata vifaa na mafundi pamoja na ushauri wa kitaalamu kuhusu masuala ya ujenzi.

Alisema Dodoma inakua kwa kasi na katika ukua huo inahitaji mafundi ambao wanafanya kazi vizuri ambapo ili kufikia lengo hilo wameamua kuwakutanisha mafundi kwa lengo la kuunda umoja wao.

Alisema lengo ni kuwaunganisha mafundi wote ili wanufaike na fursa zilizopo jijini hapa.

Naye Mwenyekiti wa Mafundi hao, Wille Sakalani, alitoa shukrani kwa ahadi zilizotolewa na mbunge huku akisema malengo yao ni kufikia hatua ya kusajili kikundi ili waweze kunufaika na fursa mbalimbali ikiwamo mikopo.





Baadhi ya wakazi wa Jiji la Mbeya wakiendelea na shughuli za uuzaji na ununuzi wa mahitaji mbalimbali kuelekea sikukuu ya Krismasi jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Maduka 25 ya mbegu yafungiwa Mbeya, Songwe

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MADUKA 25 yanayouza mbegu yamefungiwa na Taasisi ya Udhibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI), kwenye mikoa ya Mbeya na Songwe kutokana na kukiuka sheria na kufanya shughuli hiyo bila kusajiliwa.

Maduka hayo yalifungwa juzi kufuatia operesheni maalumu inayoendelea ya maofisa wa taasisi hiyo, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ya kukagua maduka mbalimbali yanayofanya biashara ya mbegu hasa katika kipindi hiki cha msimu wa kilimo.

Ofisa Mfawidhi wa TOSCI Nyanda za Juu Kusini, Peter Nassari, alisema katika operesheni hiyo walikagua zaidi ya maduka 200 na kubaini 25 yakiendelea kuuza mbegu bila kufuata taratibu.

Alisema moja kati ya taratibu ambazo wamiliki wa maduka hayo walikuwa wanakiuka ni kuuza mbegu ambazo hazijasajiliwa na kuthibitishwa ubora wake na TOSCI ambayo ndiyo taasisi iliyopewa mamlaka ya kudhibiti mbegu.

Pia, alisema baadhi ya maduka hayo yalibainika kuuza mbegu ambazo zimeingizwa nchini kutoka mataifa jirani kupitia njia za 'panya' bila kuwa na nembo ya taasisi hiyo inayoonyesha uhalali wake.

"Katika Mkoa wa Songwe pekee tulizuia zaidi ya kilo 150 za mbegu za mahindi ambazo zilikuwa zimeingizwa nchini kinyemela, na huu ukaguzi tunaendelea nao kwenye maeneo mengine ili kukomesha biashara hizi," alisema Nassari.

Nassari alisema kwa mujibu wa sheria, mtu yeyote ambaye anakamatwa kwa kukiuka taratibu za uuzaji wa mbegu, anatozwa faini ya kati ya Sh. 1,000,000 na 5,000,000 au kifungo cha kati ya miezi mitatu au mwaka au vyote viwili.

Kwa upande wake, mdhibiti wa ubora wa mbegu kutoka TOSCI, Salehe Kombo, alisema pamoja na kuchukua hatua mbalimbali dhidi ya wafanyabiashara wa mbegu wanaokiuka sheria, pia wanatoa elimu kwa wafanyabiashara na wakulima.

Alisema wanafanya hivyo kutokana na kubaini kuwa baadhi ya wafanyabiashara wanakiuka sheria bila na kwamba wanaamua kuchukua hatua zaidi baada ya kubaini kuwa baadhi ya wanaokiuka wanafanya makusudi.

Aliwataka wakulima kuhakikisha kila wanaponunua mbegu wanapewa risiti na kuzitunza ili ikitokea madhara yoyote iwe rahisi kumsaidia kwa kufuatilia kule alikonunua.

"Ukinunua mbegu bila kuchukua risiti hata sisi hatuwezi kukusaidia ukipata matatizo, lakini ukiwa na risiti inakuwa rahisi kujua mahali pa kuanzia," alisema.

Baadhi ya wakulima mkoani Mbeya, waliiomba serikali kuwachukulia hatua kali za kisheria wafanyabiashara wanaouza mbegu feki kwa kuwa vitendo hivyo vinawasababishia hasara.

Mmoja wa wakulima hao, Joseph Nkembo, ambaye ni mkazi wa Kijiji cha Utengule katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, alisema wamekuwa wakinunua baadhi ya mbegu, lakini wakip-

# Kukamilisha madarasa Januari

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya, imesema inatarajia kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza kabla ya Januari 10, mwakani ili wanafunzi ambao hawajapangiwa shule kutokana na upungufu wa vyumba waanze mapema.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliyasema hayo jana, alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu maendeleo ndani ya mkoa huo.

Alisema agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, linawataka kukamilisha vyumba hivyo kabla ya Februari 30, mwakani lakini wao wamejipanga na wamekubaliana kukamilisha kabla ya muda huo.

Alisema katika baadhi ya wilaya ikiwamo Kyela hakuna upungufu na wanafunzi wote waliofaulu wataanza masomo mapema, isipokuwa kwenye wilaya zingine kuna upungufu na wanapambana kukamilisha mapema.

"Mbali na vyumba hivyo, pia tuna mpango wa kufungua shule mpya ambazo zimekamilika, lakini kwa mwendo tunaokwenda nao nina uhakika watoto wote wataanza masomo mapema," alisema Chalamila.

Alisema moja kati ya shule mpya zitakazofunguliwa ni pamoja na za masomo ya Sayansi zitakazokuwa zinachukua wanafunzi wa kike na wa kiume.

# Mbunge ahimiza kasi ujenzi kwa muda

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MBUNGE wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza, amewataka wananchi wa Kata ya Nsalala katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi kuongeza kasi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Shule ya Sekondari Malama ili kuwezesha wanafunzi waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza mwakani, waanze masomo kwa wakati.

Njeza alitoa rai hiyo jana, wakati alipotembelea shule hiyo kukagua ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa unaoendelea shuleni hapo kwa nguvu za wananchi.

Alisema haridhishwi na kasi ya wananchi wa kata hiyo ya uchangiaji na kujitoa kwenye shughuli za maendeleo, hali inayompa shaka kama watakamilisha kazi hiyo kwa muda uliopangwa ambao ni kabla ya Januari 10 mwakani.

"Nimezunguka maeneo mengi ndani ya jimbo langu, kote nilikopita nimeona jitihada kubwa za wananchi za kujitolea kuchangia shughuli za maendeleo, hali ambayo ni tofauti kidogo na kata yenu, ninyi mko nyuma ikilinganishwa na wenzenu hivyo nawashauri ongezeni bidii ili tumalize kazi hii kwa wakati," alisema Njeza.

Katika ziara hiyo Njeza aliahidi kuchangia Sh. 2,000,000 kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa vyumba hivyo ambavyo vimefikia usawa wa mtambaa wa panya.

Awali, akisoma taarifa ya ujenzi wa vyumba hivyo, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Nsalalaa, Juma Shumba, alisema kuwa changamoto kubwa inayowakabili ni upungufu wa rasilimali fedha kwa ajili ya kukamilisha.

Shumba alisema, wamelazimika kukopa baadhi ya vifaa vya ujenzi kwa lengo la kufanikisha mapema na kuwezesha wanafunzi kuanza masomo kwa wakati.

Alivitaja baadhi ya vifaa vya ujenzi walivyokopa kuwa ni saruji, matofali na huduma ya kuletewa mawe ya msingi shuleni hapo, vyote vikigharimu zaidi ya shilingi milioni tatu.

"Tuna deni la fedha zaidi ya shilingi milioni tatu ambalo tumekopa vifaa mbalimbali vya ujenzi ili tuweze kukamilisha vyumba vya madarasa kwa wakati, tunaomba serikali itusaidie kulipa," alisema.

Shumba alisema kuwa chanzo kikuu cha mapato ya kuendesha ujenzi huo ni michango kutoka kwa wananchi, na kwamba mpaka sasa wameshakusanya fedha zaidi ya Sh. 600,000.

Alisema fedha hizo wanazitumia kuwalipa mafundi na vibarua ili kazi ya ujenzi isisimame.

Hata hivyo, Shumba alisema kuwa vyumba hivyo vikikamilika ujenzi wa maboma, watakuwa hawana fedha za kuviezeka na kuiomba serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kusaidia kazi ya kupaua.



# Rais Mwinyi asimamisha kazi watendaji mifuko ya jamii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI Mwendeshaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Sabra Issa Machano na watendaji wengine wamesimamishwa kazi kwa tuhuma za kuhusika na makosa mbalimbali katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya serikali.

Uamuzi huo ulitolewa juzi na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, wakati alipozungumza na viongozi na watendaji wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (ZAECA).

Watendaji wengine waliohusika na tuhuma hizo ni pamoja na Ramadhani Abdalla Ali na watendaji wa kamati nzima ya uratibu wa mradi wa huduma za jamii Mijini (ZUSP), kutoka Wizara ya Fedha.

Dk. Mwinyi alisema amechukua uamuzi huo kwa makosa ya kiutendaji katika utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Jumba la Treni liliopo Darajani Mjini Unguja.

Alisema ni dhahiri kuwa katika utekelezaji wa mradi huo taratibu zilikiukwa na hivyo akabinisha ulazima wa kufanyika uchunguzi, wakati watendaji hao wakiwa nje ya kazi. Alisema makosa dhidi yao hayatoi fursa ya wao kuendelea na kazi na ni vyema wakae pembeni kupisha uchunguzi na kwamba serikali itasimamia haki na kamwe hakuna mfanyakazi atakayeonewa dhidi ya tuhuma zinazowakabili.

Kadhalika, alisema hafurahishwi na utekelezaji wa mradi wa ZUSP uliogharimu Dola za Marekani milioni 93, ambao ulikusudiwa kuondoa changamoto mbalimbali katika manispaa.

Alisema taarifa zilizopo zinaonyesha kuwapo makosa makubwa katika ununuzi pamoja na kufanyika udanganyifu wa kazi zilizoelezwa kufanyika, wakati hazikufanyika.

Alisema amelazimika kuisimamisha kamati nzima ya uratibu wa mradi huo ili uchunguzi uweze kufanyika, wakati wafanyakazi hao wakiwa nje ya kazi zao.

Vile vile, Dk. Mwinyi aliagiza ZAECA kufanya uchunguzi wa kina dhidi ya mfanyakazi wa TRA, Haidar Mussa Maisara, anayetuhumiwa kushusha kiwango cha kodi katika tukio la kuingizwa bandarini kichwa cha Scania, sambamba na Kampuni ya KEVIS aliyoagiza ifanyiwe uchunguzi.

Alisema mfanyakazi huyo alijenga dhamira ya kujihusisha na rushwa na kwa nyakati tofauti aliteremsha kiwango cha kodi hiyo hadi kufikia Sh. milioni tano, fedha ambazo haziendani na thamani halisi ya kodi iliyopaswa kulipwa na hatimaye gari hilo lilitolewa usiku bila fedha hizo kulipwa.

Alisema anasikitishwa na miradi mikubwa jinsi ilivyogubikwa na matatizo makubwa kiasi ambacho haionyeshi thamani ya fedha zilizotumika na akaahidi kuchukua hatua mara moja dhidi ya wote waliokiuka kanuni za ununuzi.

Naye Mkurugenzi Mkuu ZAECA, Mussa Haji Ali, alisema pamoja na taasisi hiyo kuasisiwa katika kipindi kifupi kilichopita, imeweza kupata mafanikio makubwa katika utekelezaji wa majukumu yake makuu matatu.

Akigusia uchunguzi wa miradi mikubwa inayotokana na utekelezaji wa miradi mikubwa ya serikali, alisema ZAECA inaendelea kufanya uchunguzi katika miradi mbalimbali ikiwamo wa ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri na ukarabati wa jengo la treni ambayo imebainika kuwapo harufu za rushwa.



Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Idrisa Kitwana Mustafa, akifungua semina kwa waandishi wa habari, kuandika habari za kujenga amani na utulivu, semina hiyo iliandaliwa na klabu ya waandishi wa habari Zanzibar na kufadhiliwa na Shirika la Internews **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Makamu wa Pili atahadharisha mabadiliko tabia nchi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman, amesema kuendelea kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchini ipo haja kwa wataalamu wa sekta za mazingira kuangalia kwa kina uvamizi wa maji ya bahari yanayoendelea kukiathiri Kijiji cha Sipwese kilichopo Mkoa Kusini Pemba.

Alisema wananchi wa kijiji hicho hivi sasa wanaendelea kupata usumbufu mkubwa kutokana na sehemu wanayovukia kwenda upande wa vijiji jirani kuvamiwa na mmomonyoko wa ardhi unaosababishwa na kasi ya maji ya bahari na kuhatarisha pia maisha ya watoto wanaokwenda shule.

Alisema hayo wakati wa mazungumzo yake na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais anayesimamia masuala ya Muungano na Mazingira wa Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Ummy Mwalimu, aliyefika kujitambulisha.

Alisema Serikali ya Zanzibar imejizatiti kutoa ushirikiano wa kina kuona kero hiyo ya Sipwese inapatiwa ufumbuzi kama ilivyoshughulikiwa tatizo la athari ya tabia nchi iliyokikumba kisiwa cha Panza Pemba chini ya usimamizi wa Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano kwa ujenzi daraja na upandaji miti mambo yaliyoleta nafuu kwa wananchi wa kisiwa hicho.

Hemed alieleza kwamba yapo matumaini makubwa ya kuendelea kuimarika zaidi kwa Muungano wa Tanzania kutokana na marais wote wawili Zanzibar na Tanzania kwa kuwateua mawaziri madhubuti wenye nguvu ya kusimamia masuala ya Muungano.

Alisema hana shaka ya mawaziri hao wawili waliokwisha onyesha mwelekeo wenye matumaini mema kwa kuanza kusimamia vikao vya wataalamu na viongozi wa pande hizo mbili kuyaangalia maeneo ambayo yana dalili za changamoto za Muungano kwa pande zote mbili.

Naye Waziri wa Nchi anayeshughulikia Muungano, Ummy alisema wizara yake imepewa kazi nzito ya kuratibu masuala ya Muungano sambamba na mazingira kwa pande zote mbili.

Hata hivyo, alisema wanapaswa kuimarisha masuala ambayo yako nje ya Muungano, lakini yanajumuisha moja kwa moja miradi ya maendeleo inayotekelezwa upande wa Zanzibar ambayo inapata dhamana ya Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Alisema hatua za haraka za kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchini zimeanza kuchukuliwa hasa ikizingatiwa kwamba mazingira ya Visiwa vya Zanzibar yanalingana kwa karibu na yale yaliyopo katika mwambao wa ukanda wa mashariki mwa Tanzania Bara.

## Ataka majengo yatunzwe kudumu muda mrefu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Dk. Idrissa Muslim Hija, amewataka mafundi, wakufunzi na watawala kuwa makini katika ushughulikiaji na usimamizi wa majengo ya taasisi zao ili yadumu kwa muda mrefu zaidi.

Akizungumza jana wakati alipofungua mafunzo ya uhifadhi na uimarishaji wa majengo ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Mjini Unguja, alisema ni vyema kutofanya kazi kwa mazoea, ili kuweka ushughulikiaji mzuri wa majengo ili yawasaidie na wengine.

Dk. Idrissa alisema lengo la mafunzo hayo ni kuelewa maeneo yanayohitaji kufanyiwa matengenezo baada ya kuharibika na kuelewa matengenezo yake kwa urahisi kabla ya kuleta athari zaidi.

Aliwataka mafundi na wakufunzi hao kusikiliza vizuri mafunzo hayo, ili kuyafanyia kazi hasa wakati wa kutumia majengo yao ili lengo lifikie ufanisi katika kazi.

Dk. Idrisa alisema jengo lolote lililojengwa, ili liendelee kubaki na ubora wake linahitaji kutunzwa kwa kuhudumiwa na kuwataka kujitahidi kuyatunza vizuri ili yabakie katika uhalisia wake.

Hata hivyo, alisema wizara imefanikiwa kuunda Idara itakayoshughulikia majengo yote yaliyo chini ya Wizara ya Elimu na itakuwa na kazi ya kufuatilia kwa karibu majengo yake ya Unguja na Pemba ili panapotokea tatizo liweze kutatuliwa kwa haraka zaidi.

Naye Mkurugenzi wa Mamlaka ya Vyuo vya Amali Zanzibar, Dk. Bakari Ali Silima, aliwashukuru wakufunzi wa mafunzo hayo kwa kuamua kuwapa elimu watendaji wake juu ya usimamizi wa ukarabati na utunzaji wa majengo ya mafunzo ya amali.

Aliwataka katika mafunzo hayo kujitahidi kufahamu na kuyafanyia kazi ili lengo lililokusudiwa lifikiwe. Alisema kuwa usimamizi, utunzaji na ukarabati wa majengo ya vyuo vya mafunzo ya amali unahitaji uendelezwe, ili majengo yabaki katika ubora wake na kudumu kwa muda mrefu.

Kwa upande wao wakufunzi wa mafunzo hayo, Salum Ali Juma, kutoka Wizara ya Elimu Unguja, Khamis Rashid Mtara kutoka Wizara ya Elimu Pemba, walisema kuna umuhimu wa kufanya ukarabati wa majengo na vifaa, ili kuepusha athari kwa watumiaji pamoja na hasara zinazoweza kutokea hapo baadaye.

Walisema wanahitaji kutunza vifaa, samani au majengo kutokana na uwezo wa hali ya nchi ni mdogo ikilinganishwa na nchi nyingine, pia kuweka katika uhalisia wake, uimara pamoja na kuepusha athari.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA SHULE

Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano : 0713327613.

**OFISI ZA MATANGAZO**
Mikocheni Industial Area,
Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu Abdul Marick Katekele anatangaza kupotea kwa kadi ya gari namba T820 BQP aina ya Suzuki Escudo yenye injini namba J20A137549. Taarifa za kupotea kwa kadi zimetolewa katika kituo cha Polisi Bukoba kwa RB namba **KAG/BK/RB/624486/2020.** Yeyote atakayeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha Polisi.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu Trezguy Faustin Makona anatangaza kupotea kwa kadi ya gari namba **T 852DCM** aina ya Mark II Grand.Taarifa ya kupotea kwa kadi hiyo imetolewa katika kituo cha **Polisi Bukoba kwa RB namba KAG/BUK/RB/862947/2020.** Atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ABDALLAH MOHAMED SEIF** Anatangaza kupotelewa na Kadi ya Gari yenye namba za usajili **T924CYY** Isuzu Truck white Chassis namba **FSR33H7700D046** Engine namba **427949.** Yeyote atakayeiona atoe Taarifa Kituo chochote cha Polisi kilichokaribu
**Taarifa ya Polisi MWZ/NYA/RB/879486/2020**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JUBA TRANSORT AND WHOLE SELLER LIMITED** Anatangaza kupotelewa na Kadi ya Gari yenye namba za Usajili **T528CNU** Scania white Boxbody Chassis namba **5133449** Engine namba **6268900.** Yeyote atakayeiona atoe Taarifa Kituo chochote cha Polisi kilicho karibu
**Taarifa ya Polisi MWA/NYA/RB/879485**

Uza,
Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa
Tupigie 0782253676




OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Mamia wadaiwa kuuawa na washambuliaji Ethiopia

**Bekoji, ETHIOPIA**

ZAIDI ya watu 100 wameuawa na watu wasiojulikana Magharibi mwa Ethiopia, Tume ya Haki za Kibinadamu nchini humo imesema.

Nesi mmoja aliyekuwa akifanya kazi katika kliniki moja, aliiambia BBC kwamba zaidi ya watu 30, walikuwa wamelazwa katika kituo hicho cha afya, wengine wakiwa katika hali mahututi.

"Baadhi ya waathiriwa walipigwa, huku wengine wakichomwa visu, muuguzi huyo aliongezea".

Shambulio hilo la Jumatano katika Jimbo la Benishangul-gamuz linajili siku moja baada ya ziara ya Waziri Mkuu, Abiy Ahmed.

Katika taarifa, Tume ya Haki za Kibinadamu ya Ethioipia, ilisema kwamba shambulio hilo lilfanyika katika kijiji cha Bekoji, ambacho kipo katika eneo linaloishi raia kutoka makabila mengi.

Zaidi ya watu 100 wameuawa katika moto na ufyatulianaji wa risasi uliotekelezwa na watu waliojihami, wakati wa shambulio hilo la alfajiri, tume hiyo ilisema.

Beyene Melese, msemaji wa serikali ya jimbo hilo, alilaumu kile alichokitaja watu wasiopendelea amani kwa kutekeleza shambulio hilo.

Jumanne, Waziri Mkuu, Abiy alisafiri kuelekea katika eneo hilo ili kuzungumzia kuhusu kuzuka mara kwa mara kwa ghasia hizo za kikabila katika miezi ya hivi karibuni.

*BBC*



Wanafamilia wa Jose Garcia, aliyekufa kutokana na virusi vya corona, wakilia wakati akizikwa kwenye makaburi ya San Jose, La Mesa, New Mexico. **PICHA/REUTERS**

# Papa aahidi kuzitembelea Lebanon, Sudan Kusini haraka iwezekanavyo

**Vatican CiTY, VATICAN**

PAPA Francis ameahidi katika ujumbe wake wa Krismasi aliaoutoa jana kwamba atazitembelea nchi ya Lebanon na Sudan Kusini, mapema iwezekanavyo.

Kwa kawaida Papa huzitaja nchi katika ujumbe wake wa Siku ya Krismasi, na kuyachagua mataifa hayo mawili.

Alitoa ujumbe huo katika wa mkesha wa Krismasi kwa sababu ya shida kila moja imekumbana nayo mwaka huu.

"Nina wasiwasi sana kuona mateso na uchungu ambao umepunguza uthabiti wa asili," alisema Papa Francis.

Alieleza kwamba Lebanon, ambayo imekuwa ikipambana na shida kubwa ya kiuchumi na kutokana na bandari ya Beirut kupata mlipuko Agosti 4, mwaka huu, ambao uliua watu wapatao 200.

Alisema waathiriwa wakiwa bado wanasubiri matokeo ya uchunguzi juu ya mlipuko ulioharibu mji mkuu.

"Mapenzi yangu kwa wapendwa wa Lebanon, ambao ninatarajia kuwatembelea haraka iwezekanavyo".

Alisema alitumai nchi inaweza kusimama mbali na mzozo na mivutano ya kikanda.

Katika ujumbe tofauti ulioandikwa pamoja na Askofu Mkuu wa Canterbury, Justin Welby, ambaye ni kiongozi wa kiroho wa Ushirika wa Anglikana Ulimwenguni, na msimamizi wa Kanisa la Scotland Martin Fair, viongozi hao wa kanisa walijitolea kufanya safari kwenda kwa Wakristo wengi wa Sudan Kusini.

"Ujumbe huo ulielekezwa kwa viongozi wa Sudan Kusini, wapinzani wa zamani ambao waliunda serikali ya umoja wa kitaifa Februari, baada ya miaka ya vita vya wenyewe kwa wenyewe," uklisema ujumbe huo.

Ripoti ya Umoja wa Mataifa ilisema mwezi huu, utekelezaji wa makubaliano ya amani umekwama nchini, ambapo mafuriko Septemba yaliwahamisha mamia ya maelfu ya watu.

*REUTERS*

# Mbunge ampa talaka mkewe kisa kahamia chama cha upinzani

**West Bengal, INDIA**

UHUSIANO wa muda mrefu wa wanandoa wanasiasa katika Jimbo la India la West Bengal, umegonga mwamba huku vichwa vya habari vikisema mume atishia kumpatia talaka mkewe, aliyekuhamia chama pinzani.

Wiki hii, Saumitra Khan, mbunge kutoka Chama cha Waziri Mkuu India, Narendra Modi, kiitwacho Bharatiya Janata (BJP), alituma ilani ya talaka kwa mkewe Sujata Mondal Khan, siku moja baada ya kujiunga na chama cha Jimbo hilo Trinamol Congress Party (TMC).

Jimbo la West Bengal, linajiandaa kwa uchaguzi mdogo katika kipindi cha miezi michache na kinyanganyiro kikuu ni kati ya BJP na TMC.

Katika mkutano na waandishi wa habari katika mji wa jimbo hilo Kolkata, siku ya Jumatatu, Mondal Khan, alitangaza uamuzi wake kukihama Chama cha BJP huku akitoa sababu kadhaa za hatua yake.

Alisema kwamba chama hicho hakikumpa heshima na kwamba kiliwakaribisha viongozi kadhaa wafisadi kutoka vyama vingine na kuahidi kuwazawadia bila ya kutilia maanani wanachama watiifu.

"Chama cha BJP kimekuwa Trinamol ndogo. Hivyo basi kwa nini nisalie katika chama hicho? Kwa nini nisiende katika timu kubwa ya Trinamol TMC?" Alisema.

Saa chache baadaye, katika mkutano ulioitishwa kwa haraka, ambao waandishi wa habari walitaja kuwa uliokumbwa na viroja.

Khan, mwenye umri wa miaka 40, alizuia machozi huku akionyesha uchungu wake na kutoa hasira wakati akitangaza uamuzi wake wa kukata uhusiano wa miaka 10 na mkewe.

*BBC*

# Trump apinga muswada wa bajeti ya ulinzi

**Washington, MAREKANI**

RAIS Donald Trump, amepiga kura ya kupinga muswada wa bajeti ya ulinzi nchini Marekani.

Trump, amepiga kura ya kupinga Sheria ya Uidhinishaji wa Ulinzi wa Kitaifa (NDAA), ambayo imetenga dola bilioni 740 kwa bajeti yake.

Katika barua aliyoituma kwa Baraza la Bunge, Trump alisema kwamba alipiga kura ya kupinga NDAA, ambayo iliwasilisha idhini baada ya kukubaliwa katika Seneti na Baraza la Wawakilishi.

"Kwa bahati mbaya, muswada huu hauna masuala muhimu ya usalama wa kitaifa na unapingana na hatua zangu za usalama wa kitaifa pamoja na sera za kigeni ambazo nilizipa kipaumbele Marekani.

Muswada huu ni zawadi kwa China na Urusi," alisema Trump.

Muswada huo, ambao ulipitishwa na Baraza la Wawakilishi na Seneti kwa zaidi ya kura mbili kwa tatu, utarejeshwa tena bungeni na kura ya Trump inaweza kubatilishwa ikiwa utapitishwa kwa idadi hiyo hiyo. Muswada huo unajumuisha, suala la mfumo wa ulinzi wa anga wa S-400 uliopokewa na Uturuki kutoka Urusi, hatua za vikwazo dhidi ya maadui wa Marekani kupitia Sheria ya Ugaidi (CAATS).

Pia unajumuisha operesheni muhimu na Urusi kama inavyokubalika ndani ya siku 30 baada ya sheria kutawaliwa, maamuzi ya vikwazo vya CAATSA kwa Uturuki na kwa wale waliohusika katika ununuzi wa S-400.

TRT

# ERIKSEN AWEKWA ORODHA YA WANAOONDOKA INTER

**MILAN, Italia**

CHRISTIAN Eriksen amewekwa kwenye orodha ya wachezaji wanaoondoka Inter Milan wakati wa dirisha dogo la Januari, amethibitisha Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Giuseppe Marotta.

Eriksen aliigharimu Inter euro milioni 20 mwanzoni mwa mwaka huu baada ya kukataa kusaini mkataba mpya kule Tottenham Hotspur.

Huku akiwa anaonekana hana nafasi kwenye kikosi cha Spurs, ilionekana kwenda kwake Inter kungemfanya kuwa na furaha, lakini aliweza kuanza mechi nane tu za Ligi Kuu Italia, Serie A, mwishoni mwa msimu uliopita wa 2019-20.

Hajaweza kumshawishi Kocha Mkuu wa Inter, Antonio Conte, msimu huu kwani ameanza katika mechi nne tu za Ligi Kuu msimu wa 2020-21.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Denmark amecheza mechi nne zaidi akitokea benchi, akipiga shuti moja tu kwa kipindi cha dakika 276 alizokuwa dimbani.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 hakuwekwa kwenye kikosi cha Inter kwa ajili ya mchezo wa Serie A dhidi ya Hellas Verona, juzi Jumatano, huku Marotta akibainisha ameshacheza mechi ya mwisho wa klabu hiyo.

"Naweza kuthibitisha kwamba, Christian Eriksen yupo kwenye orodha ya wachezaji wanaondoka," alisema akiiambia Sky Sport Italia.

"Ataondoka Januari. Hajaweza kufiti kwenye mipango yetu, alikuwa na wakati mgumu hapa Inter.

"Nafikiri ni jambo muhimu kwa Christian kuondoka na kwenda sehemu nyingine kutafuta nafasi zaidi ya kucheza."

# THIAGO AANZA MAZOEZI LIVERPOOL

**LIVERPOOL, England**

THIAGO Alcantara anakaribia kurudi uwanjani katika kikosi cha Liverpool baada ya kuanza mazoezi na kikosi cha kwanza.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania amekosa zaidi ya miezi miwili tangu alipoumia goti kwenye mchezo wa 'dabi' ya Merseyside ya Everton iliyochezwa Oktoba 17, mwaka huu.


Pia alikuwa na virusi vya corona, na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 amecheza mara mbili tu kwa Liverpool tangu alipowasili hapo akitokea Bayern Munich kwa dili liilogharimu kasi cha pauni milioni 25.

Baada ya kujifua mwenyewe, Thiago aliposti picha Jumatano kwenye ukurasa wake wa Twitter akithibitisha kwamba kuanza mazoezi na kikosi kizima.

Aliweka picha akiwa mazoezini na kuandika: "Nimerudi."

Thiago alionyesha mchango wake mzuri wakati alipoanza kucheza dhidi ya Chelsea Oktoba 20, mwaka huu.



# OZIL: BADO NAIPENDA SANA ARSENAL

**LONDON, England**

LICHA ya kutemwa kikosini na Kocha, Mikel Arteta, Mesut Ozil amesema bado ana mapenzi na klabu ya Arsenal.

Ozil haijaitumikia Arsenal tangu Machi 7, mwaka huu na hayupo kwenye kikosi cha Arsenal kinachoshiriki michuano yoyote msimu huu.

Licha ya kiungo huyo angeweza kuondoka klabuni hapo, bado anasimamia msimamo wake wa kutumikia mkataba wake mpaka mwisho.


Kutocheza mchezo wowote hakumfanyi Mesut kupunguza mapenzi yake kwa klabu hiyo.

Baada ya Arsenal kutolewa katika hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la Carabao mchezo ambao umekamilisha vipigo sita ndani ya michezo 11, Bado Mesut anaamini atapata nafasi kwenye kikosi hicho kinachotaabika kwa matokeo mabaya msimu huu.

Kupitia ukurasa wake wa Twitter, Mesut ameandika; "Ni wakati mgumu kwa kila mtu kwenye klabu, sio mimi tu.

"Ni kweli ninatamani ningeweza kuisaidia timu hasa wakati huu, lakini kutokana na kwamba sipewi nafasi, ninaimani tutapata matokeo mazuri siku chache zijazo."

## HABARI MICHEZO



# TRIPPIER AFUNGIWA MECHI 14

**LONDON, England**

MLINZI wa Atletico Madrid na England, Kieran Trippier, amefungiwa kwa wiki 10 kujishughulisha na soka na anatakiwa kulipa faini ya pauni 70,000 kwa kukiuka sheria za Chama cha Soka cha England (FA), kutokana na kujihusisha na michezo ya kubashiri.

Tamko la FA limethibitisha juu ya uamuzi huo wa kumsimamisha kwa wiki 10.

Nyota huyu mwenye miaka 30 hatatakiwa kushiriki kwenye shughuli zozote za kimichezo mara tuu baada ya hukumu hiyo kutoka, na adhabu yake itadumu hadi Februari 28, mwakani.

Trippier alikuwa anatuhumiwa kwa makosa saba yanayohusiana na kukiuka vipengele vya masharti ya sheria za FA za Julai, 2019.

Katika makosa hayo aliweza kukana makosa yote, lakini makosa manne yalipatikana kuwa na ushahidi na kupelekea uamuzi wa adhabu hiyo.

Kutokana na adhabu hiyo, nyota huyo atakosa takribani mechi 14 za LaLiga, na mechi moja ya mzunguko wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya mtoano wa timu 16 dhidi ya Chelsea.

Kwa maana hii, Trippier anatarajia kurejea tena dimbani wakati Atletico wakiwakaribisha Real Madrid, Machi 7, mwakani.

# ADHABU YA RABIOT YAZUA UTATA SERIE A



**TURIN, Italia**

KUMEKUWA na mkanganyiko juu ya adhabu aliyopewa Adrien Rabiot ya kufungiwa mechi baada ya Napoli kushinda rufani yao ya ushindi wa mezani.

Rabiot alipaswa kuikosa mechi dhidi ya Napoli ambayo ilikuwa ni adhabu ya wiki ya tatu ya mechi.

Kwa kuwa Juventus walipewa ushindi wa mezani wa mabao 3-0, huku Napoli wakipokonywa pointi, Rabiot alihesabiwa tayari alikuwa amemaliza adhabu yake aliyopaswa kuitumikia siku hiyo.

Hata hivyo, baada ya Napoli kukata rufani na kushinda rufani yao, na mechi dhidi ya Juventus kutakiwa kurudiwa, Rabiot anatakiwa kutumikia adhabu yake.

Kwa mujibu wa Juventus, klabu iliamua kumwacha kwenye mechi dhidi ya Fiorentina ya Jumanne, ikiwa ni siku ambayo hukumu ya rufani ya Juventus ilitoka.

Sababu ya kuachwa ikihusishwa na adhabu aliyopaswa kuitumikia.

Hata hivyo, kwa mujibu wa La Gazzetta dello Sport, adhabu hiyo inapaswa kutumikiwa na nyota huyo kuanzia siku inayofuata ya hukumu kutolewa.

Hii ikimaanisha kuwa bado Rabiot atapaswa kuikosa mechi inayofuata dhidi ya Udinese, Januari mwakani.

Kama suala hili litapewa uzito kwa upande huu, basi ataikosa pia mechi ijayo.



# BADO UCHUNGUZI WAENDELEA KIFO CHA MARADONA

**BUENOS AIRES, Argentina**

LICHA ya gwiji wa soka wa Argentina, Diego Maradona kuzikwa zaidi ya mwezi mmoja uliopita, lakini uchunguzi juu ya kifo chake bado unaendelea.

Maradona alifariki kwa mshtuko wa moyo ikiwa ni wiki moja baada ya kufanyiwa operesheni ya kuondoa uvimbe kwenye ubongo.

Baada ya kifo chake mwili wake ulifanyiwa uchunguzi kuhusiana na madai kuwa huenda kliniki iliyokuwa ikimhudumia matibabu ilihusika kusababisha kifo chake.

Licha ya kuwa bado hakujapatikana ushahidi wa moja kwa moja juu ya tuhuma hizo, bado uchunguzi unaendelea kubaini undani wa sakata hili.


Taarifa ya awali ilibainisha kwamba, Maradona hakutumia pombe au dawa yeyote kabla ya kifo chake.

Kifo cha Maradona huyu kinahusishwa na tatizo la moyo ambalo hupelekea moyo kushindwa kufanya kazi ghafla.

Uchunguzi ulikuwa unahusisha kubaini pia kama kuna uzembe ulifanyika na kuwajibika kwa namna yeyote kwa kliniki ambayo awali pia ilipekuliwa na vyombo vya usalama.

Ushahidi haujaweza kutosheleza kuwajibisha upande wa wahudumu wake wa afya, na uchunguzi bado unaendelea kubaini zaidi undani wa sakata hili.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# CAVANI ATAJWA KUIBEBA UNITED

**Ni kauli iliyotolewa na Solskjaer baada ya straika huyo wa Uruguay kuing'arisha timu hiyo...**

**LIVERPOOL, England**

OLE Gunnar Solskjaer amesifia "mchango mkubwa" wa Edinson Cavani katika kikosi cha Manchester United baada ya kufanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la EFL.

Cavani alifunga bao kwa shuti kali dakika ya 88 kabla ya Anthony Martial kuiwezesha United kupata ushindi wa 2-0 dhidi ya Everton pale kwenye dimba la Goodison Park, juzi Jumatano.

Bao hilo la mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay lilikuja wakati akipiga shuti lake la nne kwenye mchezo huo, ambapo yeye binafsi alikuwa na mashuti mengi zaidi yaliyolenga goli kuliko timu nzima ya Everton.

Cavani amefunga mabao manne katika mechi 12 kwa United msimu huu na Solskjaer akamsifia straika huyo, huku akipuuzia madai kwamba, nyota huyo mwenye umri wa miaka 33 alianza taratibu klabuni hapo.

"Nafikiri hauko sawa, sidhani kama alianza taratibu. Nafikiri amefanya vizuri sana," amesema kocha huyo wa United akiwaambia waandishi wa habari.

"Alikuwa ameumia, yoyote anaweza kuumia. Alikuja amechelewa kwenye dirisha la usajili, hivyo nimefurahishwa sana na mchango wake kwenye timu.

"Kwenye vyumba vya kubadilishia nguo, tabia yake ni nzuri na anahamasisha mazoezi, akili yake ni kwenye mchezo. Unaweza kuona namna gani anavyojiangalia yeye na timu.

"Alifunga mabao muhimu sana kwa upande wetu na imetupa uzoefu wa kutosha. Yeye atakuwa hapa na atakuwa bora na bora zaidi kwa sababu alikuwa nje ya dimba kwa miezi saba.

"Tumekuwa na subira juu yake na nafikiri imeleta mchango mkubwa sana." Wakati Cavani na Martial wakiipeleka United hatua ya nusu fainali ambapo watakutana na Manchester City, Paul Pogba alionyesha kiwango cha kuvutia zaidi.

## KWA UFUPI

**CHELSEA YAINGIA VITANI**

CHELSEA imejiunga katika kinyang'anyiro cha kuwania kumsajili mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 20, lakini Manchester City inajichukulia ndio ilio kifua mbele kunasa saini ya mchezaji huyo. ***(90 min)***

**CALVERT-LEWIN SOKONI**

MATUMAINI ya Manchester United kumsajili Erling Halaand huenda yakadhoofishwa kutokana na uhusiano wake na wakala Mino Raiola, na sasa mshambuliji wa Everton, Dominic Calvert-Lewin mwenye umri wa miaka 23, anatajwa kuwa mbadala katika kikosi hicho cha Ole Gunnar Solskjaer. ***(Mirror)***

**PSG YAMTAKA LUDIGER**

PARIS St-Germain inamnyatia Antonio Rudiger mwenye umri wa miaka 27, huku beki huyo akiwa hana nafasi kwenye kikosi cha kwanza cha Chelsea pale Stamford Bridge. ***(Le Parisien - in French & subscription required)***

**MILITAO ANUKIA LIVERPOOL**

LIVERPOOL ina hamu ya kumsajili beki wa Real Madrid, Eder Militao mwenye umri wa miaka 22, huku mchezaji wa Argentina, Ezequiel Garay (34), akitarajiwa kujiunga na klabu hiyo iliyoko chini ya kocha Jurgen Klopp. ***(Todofichajes)***

**ARSENAL YAMFUATA VINICIUS JR**

MIKEL Arteta na Arsenal wameonyesha nia ya kutaka kumsajili kwa mkopo mshambuliaji wa Real Madrid na Brazil, Vinicius Jr mwenye umri wa miaka 20, wakati wa dirisha dogo la Januari. ***(Daily Star)***

**MUSTAFI ANUKIA BARCA**

BARCELONA imeanza mazungumzo na beki wa Arsenal na Ujerumani, Shkodran Mustafi mwenye umri wa miaka 28 ili kumsajili kwa uhamisho huru, mara mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(SPOX via 90 min).***

**ROONEY AMTAKA JONES**

KOCHA wa Derby County, Wayne Rooney anataka kumsajili mlinzi wa Manchester United na Timu ya Taifa ya England, Phil Jones mwenye umri wa miaka 28. ***(Metro)***

**KARIUS KURUDI LIVERPOOL**

GOLIKIPA, Loris Karius (27), huenda akarudi katika klabu yake ya Liverpool baada ya Union Berlin kufikiria kusitisha mkataba wake mapema, huku mchezaji huyo wa Ujerumani akichezeshwa mara moja tangu kuanza kwa msimu. ***(Kicker via The Sun)***

**BARCA KUMBANA PUIG**

BARCELONA inajaribu kutaka kumshawishi kiungo wake, Ruqui Puig kutia saini mkataba mpya, huku nyota huyo mwenye umri wa miaka 21 akiwa anawaniwa na Manchester City pamoja na Bayern Munich. ***(Fichajes)***

**BAJCETIC KUTUA LIVERPOOL**

LIVERPOOL inajiandaa kumsajili beki wa Celta Vigo, Stefan Bajcetic (16), chini ya mwamvuli wa Manchester United, ingawa mchakato wa kukamilisha utatakiwa kukamilika kabla ya dirisha la usajili ya Januari halijafunguliwa. ***(Liverpool Echo)***

**LINGARD MAMBO SAFI**

MANCHESTER United inataka kumpa mkataba mpya wa miezi 12 nyota wake, Jesse Lingard ambao utamalizika ifikapo mwaka 2022, ili kumzuia winga huyo mwenye umri wa miaka 28 kuondoka kama mchezaji huru kipindi cha majira ya joto mwakani baada ya mkataba wake wa sasa kumalizika. ***(Mail)***

HABARI MICHEZO

# HITIMANA JUKWAANI MTIBWA IKICHAPWA

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA mpya wa Mtibwa Sugar, Thiery Hitimana, bado hajaanza kuifundisha timu hiyo kutokana na kutokamilika kwa taratibu za vibali na kushuhudia kikosi chake kikifungwa bao 1-0 na Dodoma Jiji FC kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani Morogoro juzi.

Hitimana aliliambia gazeti hili bado hajaanza kukaa kwenye benchi la timu hiyo mpaka pale taratibu husika zitakapokamilika.

Ofisa Habari wa Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru, alisema sababu zilizofanya kocha wao achelewe kuanza kazi na kukaa kwenye benchi ni kutaka kuangalia mazingira ya klabu hiyo na endapo ataridhika ndio watakamilisha mazungumzo.

Kifaru alisema kuna baadhi ya taratibu bado hazijakaa vyema ingawa wanaamini baada ya sikukuu ya Krismasi kupita, zitakamilika.

"Unajua makubaliano yetu ya mwanzo yalikuwa ni Dar es Salaam, lakini baada ya hapo tukamwambia kabla hatujamalizana kabisa twende ukaone klabu yetu ilipo, makao makuu yetu na mazingira yote ili kama akikubaliana nayo ndipo tumalizane moja kwa moja, huwezi kumalikana na mtu bado hajaangalia mazingira ya eneo lake la kufanyia kazi jinsi lilivyo," alisema Kifaru.

Hivi karibuni, klabu hiyo ilimtangaza Hitimana kuchukua mikoba ya aliyekuwa Kocha Mkuu, Zuberi Katwila baada ya kuona mambo hayaendi vyema tangu kuanza kwa msimu.

Wakati wa mazungumzo na Hitimana yakielekea ukingoni, Mtibwa Sugar inaendelea kuongozwa na Kaimu Kocha Mkuu, Vicent Barnabas.

Timu hiyo imemaliza mzunguko wa kwanza ikiwa kwenye nafasi ya tisa baada ya kujikusanyia pointi 22 wakati Yanga yenye pointi 43, ndio vinara wa ligi hiyo huku mabingwa watetezi Simba iliyocheza mechi tatu pungufu ikifuata kwenye msimamo.




Kipa wa Al Hilal Elobied ya Sudan, Yonis Hassan, akipangua hatari kwenye lango lake katika mchezo wa mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Namungo FC uliochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini, Dar es Salaam juzi. Namungo ilishinda mabao 2-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Yondani atajwa kuibeba Polisi

**Na Saada Akida**

BAADA ya kukamilisha usajili wa aliyekuwa beki tegemeo wa Yanga, Kelvin Yondani, Kocha Mkuu wa Tanzania Polisi, Malale Hamsini, kikosi chake kinatarajia kupata mambo mazuri kutoka kwa nyota huyo huku akitamba safu yake ya ulinzi itakuwa imeimarika.

Malale aliliambia gazeti hili jana tayari wamekamilisha mchakato wa kumsajili beki huyo kwa kumpa mkataba wa miezi sita na hivyo anaingia moja kwa moja kwenye mipango yake.

Kocha huyo alisema Yondani ni miongoni mwa wachezaji aliowapendekeza katika ripoti yake ya usajili wa dirisha dogo, ili kuimarisha kikosi chake na anafurahi kufanikiwa kumpata.

"Yondani ni mchezaji mzuri, ana uzoefu na Ligi Kuu Tanzania Bara, nina imani atatusaidia sana katika harakati zetu za kupambana kufanya vizuri msimu huu," alisema Malale.

Aliongeza safu yake ya ulinzi ilikuwa na upungufu na kupatikana kwa Yondani ambaye atashirikiana na mabeki wengine waliokuwapo ndani ya timu hiyo kutasaidia kufanya vizuri kwenye mechi zitakazofuata.

Yondani amejiunga na Polisi Tanzania akiwa ni mchezaji huru baada ya mkataba wake na Yanga kumalizika baada ya msimu wa 2019/20 kukamilika.

## Straika Namungo aahidi makubwa

**Na Saada Akida**

STRAIKA wa Namungo FC, Sixtus Isabilo, amesema wataenda Sudan kutafuta matokeo mazuri katika mechi ya marudiano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Al Hilal Elobied itakayochezwa Januari 5, mwakani jijini Khartoum.

Namungo ilianza vyema hatua ya kwanza baada ya juzi kupata ushindi wa mabao 2-0 na hivyo kujiweka katika mazingira mazuri ya kusonga mbele.

Akizungumza na gazeti hili jijini, Dar es Salaam jana, Isabilo alisema wamejipanga kwenda kupambana kwa sababu wanatarajia kukutana na mechi ngumu na yenye ushindani.

Isabilo alisema licha ya ushindi waliopata, bado kocha wao, Hemed Morocco ataendelea kuyafanyia kazi upungufu uliyojitokeza katika mechi hiyo ya kwanza, ili watakapofika ugenini wapate matokeo changa na kusonga mbele katika michuano hiyo.

"Hii mechi ilikuwa na ushindani mkubwa, kipindi cha pili wenzetu walibadilika, tuna imani mechi ya marudiano itakuwa ya ushindani zaidi kwa sababu wenzetu watakuwa nyumbani kwao, wanahitaji kupata matokeo chanya halikadhalika na sisi tunaenda kupambana," alisema Isabilo.

Naye Mwenyekiti wa Namungo FC, Hassan Zidadu, alisema uongozi wa timu hiyo utakutana hivi karibuni ili kuandaa mipango ya kujiimarisha kuelekea mchezo wa marudiano.

## Women Fighter, Jumbi kibaruani

**Na Hawa Abdallah**

TIMU ya Women Fighter inatarajia kuanza kampeni ya kuwania ubingwa wa Kombe la Mapinduzi kwa kuwakaribisha Jumbi Queens katika mechi ya ufunguzi wa mashindano itakayofanyika leo kwenye Uwanja wa Mau Visiwani hapa.

Hii ni mara ya kwanza kwa soka la wanawake kuwapo kwenye mashindano ya Kombe la Mapinduzi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Kamati ya Soka la Wanawake ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Nasra Juma, alisema michuano hiyo inatarajiwa kuchezwa katika viwanja vya mitaani ili kuleta hamasa katika soka la wanawake ambalo bado liko chini kwa Zanzibar.

Nasra alisema jumla ya timu tisa kutoka Unguja, zinatarajiwa kuchuana kuwania ubingwa wa michuano hiyo baada ya klabu za Pemba kushindwa gharama za usafiri.

Kiongozi huyo alizitaja timu zitakazoshiriki mashindano hayo ni pamoja na Yellow Queens, New Sister, Future Queens , Ladies Fighters, Amani Queens, Women Fighter, New Generation, Green Queens na Jumbi Women Fighter.

Alimtaja Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Mwita, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika ufunguzi wa michuano hiyo kwa upande wa wanawake.

# Michezo

Ijumaa Desemba 25, 2020

Nipashe




## CAVANI ATAJWA KUIBEBA UNITED

HABARI UK 22



Mshambuliaji wa Manchester United Mfaransa, Anthony Martial (kushoto), akifunga bao la pili katika mechi ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la Ligi nchini England dhidi ya Everton iliyochezwa kwenye Uwanja wa Goodison Park juzi usiku. United ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

## SIMBA: KAZI BADO

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kikosi chake kukubali kichapo cha bao 1-0 FC Platinum ugenini Harare nchini, Zimbabwe, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck amesema hajafurahishwa na matokeo hayo hivyo wanahitaji kuongeza umakini kuelekea mchezo wa marudiano.

Simba inatarajia kuwakaribisha Wazimbabwe hao katika mechi ya marudiano ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa Januari 6, mwakani kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam.

Sven alisema wachezaji wake walianza vyema mchezo huo lakini baadaye walipoteza umakini jambo ambalo litawafanya wabadilike katika mchezo wa marudiano ambao utaamua hatima yao kwenye michuano hiyo.

"Tunapaswa kuwa makini zaidi kwenye mchezo wa marudiano kwa sababu tulistahili kushinda kwenye mchezo wetu ambao tulitawala kwa asilimia kubwa.

"Sijafurahishwa na matokeo ambayo tumeyapata ugenini hivyo tuna kazi ya kufanya katika mchezo wetu wa nyumbani," alisema Mbelgiji huyo. Bao pekee la FC Platinum katika mchezo huo uliochezwa kwenye Uwanja wa Taifa mjini Harare lilifungwa dakika ya 17 na Perfect Likwende.

# YANGA: TUNA JAMBO LETU

## ●●●Pia yafunguka kuendelea kudai haki dhidi ya Morrison, yasonga mbele FA...

**Shufaa Lyimo na Nebart Msokwa, MBEYA**

WAKATI Kocha Msaidizi wa Yanga, Juma Mwambusi, akisema lengo lao kubwa msimu huu ni kuona wanatwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, kesi kati ya klabu hiyo na mshambuliaji wa Simba, Bernard Morrison imefufuka upya.

Akizungumza na gazeti hili jana baada ya timu yao kumaliza mzunguko wa kwanza bila kupoteza mchezo hata mmoja, Mwambusi alisema wamefurahishwa na kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wao katika mechi za hivi karibuni.

Mwambusi alisema msimu huu umekuwa na ushindani zaidi, lakini mbinu na mikakati ambayo wanawapa wachezaji wao, imesaidia kupata matokeo mazuri katika mechi mbalimbali walizocheza.

Kocha huyo alisema wachezaji wao wameendelea kuimarika na wanaonekana wako tayari kupambana ili kufikia malengo waliyojiwekea msimu huu.

"Tunashukuru kwa matokeo ambayo tunaendelea kuyapata, malengo yetu ni kuwa mabingwa msimu huu, hatuna lingine, tumejiandaa kurejesha heshima Jangwani," alisema Mwambusi.

Aliongeza mazoezi ambayo wanawapa wachezaji wao, yamesaidia kupandisha viwango vyao na sasa wanaamini kila timu watakayokutana nayo ijiandae kupokea kichapo.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, alisema matokeo waliyopata katika mechi ya juzi yametokana na kikosi imara walichonacho na si vinginevyo.

Mwakalebela alisema Yanga ina kila sababu ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu kutokana na juhudi mbalimbali zinazofanywa na wachezaji wao.

Alisema katika kuhakikisha inajiimarisha zaidi, kikosi cha timu yao kitaendelea kuweka kambi jijini Mbeya, ili kujiandaa na mchezo wake wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Tanzania Prisons utakaochezwa Desemba 30, mwaka huu kwenye Uwanja wa Nelson Mandela mkoani Rukwa.

"Tunamshukuru Mungu mchezo wetu wa jana (juzi) dhidi ya Ihefu ulimalizika salama na tukaibuka na ushindi ambao umetufanya tumalize mzunguko wa kwanza bila kufungwa mchezo wowote, sasa tunawaomba wapenzi na mashabiki wa timu yetu waendelee kutupatia ushirikiano kwa muda wote tutakaokuwapo hapa Mbeya," alisema Mwakalebela.

Hata hivyo Mwakalebela alikiri kuwa msimu huu ni mgumu kuliko misimu iliyopita na hivyo akawataka wapenzi na mashabiki wa timu hiyo kuendelea kuipa ushirikiano timu yao.

Wakati huo huo, Mwakalebela alisema Yanga itaendelea kudai haki yake dhidi ya aliyekuwa mchezaji wao, Morrison kwa kulipa kiasi cha fedha zilizotakiwa na Mahakama ya Usuluhishi ya Kimataifa (CAS), baada ya kukata rufani kufuatia kutoridhishwa na hukumu iliyotolewa na Kamati ya Sheria na Hadhi ya Wachezaji ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

Kiongozi huyo alisema Yanga itakuwa tayari kumlipia Morrison ada iliyotakiwa ili kuhakikisha shauri hilo linasikilizwa na hatimaye haki ionekane imetendeka.

"Fifa imesema kuwa maelezo ambayo aliyatoa mlalamikiwa (Morrison), hayana mashiko hivyo kesi itaendelea kusikilizwa na haki itatendeka. Inatakiwa kulipa fedha kwa pande zote mbili ili kesi isikilizwe na kiasi ambacho kinatakiwa ni fedha za Kifaransa 12,000, mlalamikaji na mlalamikiwa anapaswa kulipa.

"Sisi tumedhamiria kulipa fedha hizo ili kesi iweze kusikilizwa na jukumu letu ni kuona kwamba kila upande una kazi ya kulipa fedha hizo na ikiwa upande mmoja utashindwa kulipa basi kesi itafutiliwa mbali," Mwakalebela alisema.

Katika hatua nyingine, Yanga imekuwa timu ya kwanza kutinga raundi ya nne ya mashindano ya Kombe la Shirikisho baada ya wapinzani wao, Singida United iliyokuwa inashiriki Ligi Daraja la Kwanza kushushwa madaraja mawili sambamba na matokeo yake kufutwa baada ya kutotokea kwenye mechi yake dhidi ya Alliance FC katika ligi hiyo.

Taarifa kutoka TFF imesema mchezo huo uliotarajiwa kuchezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa hautachezwa tena.

"Hivyo Young Africans sasa wanasubiri kucheza raundi ya nne 2021," ilisema sehemu ya taarifa ya TFF.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002